



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



## TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2020

KISWAHILI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA  
WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA  
KIDATO CHA NNE (CSEE) 2020**

**021 KISWAHILI**

*Kimechapishwa na:*  
Baraza la Mitihani la Tanzania,  
S.L.P. 2624,  
Dar es Salaam,Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

## **YALIYOMO**

DIBAJI.....	iv
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI.....	2
2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA .....	2
2.1.1 Swalii la 1: Kuchagua.....	2
2.1.2 Swalii la 2: Kuoanisha.....	13
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI.....	16
2.2.1 Swalii la 3: Aina za Maneno. ....	17
2.2.2 Swalii la 4: Aina za Maneno .....	20
2.2.3 Swalii la 5: Matumizi ya Lugha .....	23
2.2.4 Swalii la 6: Uhakiki wa Riwaya .....	26
2.2.5 Swalii la 7: Uhakiki wa Ushairi.....	30
2.2.7 Swalii la 8: Uandishi .....	35
2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU .....	40
2.2.8 Swalii la 9: Ukuaji na Ueneaji wa Kiswahili Baada ya Uhuru.....	40
2.2.9 Swalii la 10: Uhakiki wa Ushairi.....	45
2.2.10 Swalii la 11: Uhakiki wa Riwaya .....	52
2.2.11 Swalii la 12: Uhakiki wa Tamthiliya .....	58
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA .....	64
4.0 HITIMISHO .....	65
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO.....	66
KIAMBATISHO A .....	67
KIAMBATISHO B .....	68

## **DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania lina furaha kutoa taarifa hii kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne mwaka 2020 kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera na wadau wengine wa elimu kwa ujumla kuhusu wanafunzi walivyojibu maswali katika mtihani huu.

Taarifa hii inalenga kutathmini muhtasari wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne ili kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu hususan katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi, majibu ya watahiniwa yanalenga kuonesha dhahiri mambo ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa katika elimu ya Sekondari kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuelewa sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani huu. Taarifa hii inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kufanya vizuri au kwa kiwango cha wastani. Sababu hizo ni pamoja na uelewa wa mada zilizotahiniwa, uelewa wa matakwa ya swali na uwezo wa kujieleza kwa kutumia lugha fasaha ya Kiswahili. Aidha, sababu zilizofanya baadhi ya watahiniwa kupata alama hafifu zimefanuliwa. Sababu hizo ni kama vile; kutokuelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kujieleza kwa lugha fasaha na kutokuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili. Mrejesho huu, utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu mwafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kutayarisha ripoti hii.



Dr. Charles Msonde

## **KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2020 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huu ulikuwa na maswali 12 yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C. Mada zilizotahiniwa katika sehemu zote zilihuisha *Ufahamu, Matumizi ya Sarufi na Utumizi wa Lugha, Uandishi, Maendeleo ya Kiswahili, Uundaji wa Maneno* pamoja na *Fasihi*. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali matatu (3) kutoka sehemu C.

Watahiniwa (**437,589**) walifanya mtihani wa somo la Kiswahili kwa mwaka 2020. Kati yao, watahiniwa **413,066** sawa na asilimia **94.83** walifaulu kwa kupata daraja A hadi D. Kwa ujumla, ufaulu huo ni wa juu kwa asilimia **3.52** ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa **91.31**. Ufaulu wa watahiniwa kwa kila daraja umeoneshwa katika **Jedwali Na. 1**.

Mwaka	Waliofanya	Madaraja				
		A	B	C	D	F
2019	424,843	10,686	56,461	216,159	102,486	36,730,
2020	437,589	22,198	75,774	235,949	79,145	22,505

**Jedwali Na. 1:** Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Daraja kwa Mwaka 2019 na 2020

Uchambuzi umefanyika kwa kuzingatia namna maswali yalivyojibiwa, jinsi yalivyopaswa kujibiwa na changamoto zilizojitokeza. Vilevile, uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni *vizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha ufaulu kimeanzia alama 65 hadi 100, wastani alama 30 hadi 64 na kiwango hafifu alama 0 hadi 29. Aidha, chati na majedwali mbalimbali yanetumika ili kufafanua viwango hivyo ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ikiwakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ikiwakilisha ufaulu hafifu. Hata hivyo, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatishwa ili kutoa ufanuzi zaidi.

Kwa ujumla, uchambuzi huu unalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu ili kuweka mkakati wa kuinua kiwango cha ufaulu kwa vizazi vijavyo.

## **2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI**

Sehemu hii inafafanua uchambuzi wa kina wa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanyika kwa kiwango kizuri, cha wastani na yale yaliyofanyika kwa kiwango hafifu. Aidha, sababu za ufaulu wa watahiniwa katika viwango hivyo zimeelezwa bayana kwa kila swali. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huo.

### **2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA**


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua likiwa na vipengele kumi (10) na swali la 2 lilikuwa la kuoanisha likiwa na vipengele vitano (5). Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

#### **2.1.1 Swali la 1: Kuchagua**

Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuelewa dhana mbalimbali zinazohusu mada anuwai za somo la Kiswahili. Swali lilihusu mada za *Aina za maneno*, *Utumizi wa Lugha*, *Fasihi simulizi*, *Mjengo wa Tungo*, *Kuongeza Msamiati wa Kiswahili na Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A - E) kwa kila kipengele. Aidha, jumla ya alama katika swali hili zilikuwa 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Watahiniwa 435,681 sawa na asilimia 99.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Watahiniwa 317,611 sawa na asilimia 72.9 walifaalu kwa kiwango cha wastani hadi

kizuri hivyo, kufanya swali hili kuwa mionganini mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 1:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1

Katika Chati Na. 1, watahiniwa 117,900 (27.1%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5, watahiniwa 263,884 (60.5%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na watahiniwa 53,897 (12.4%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi alama 10.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 60.5 ya watahiniwa walijibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa dhana zilizotahiniwa kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Hivyo walimudu kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele 3 - 6 na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache (12.4%) walijibu vizuri swali hili kwa kuwa walikuwa na umahiri pamoja na uelewa wa dhana katika mada zilizotahiniwa. Kwa ujumla, watahiniwa hao waliweza kujibu vipengele vingi vya swali hili, haswa kwa kumudu kuchagua herufi yenye jibu sahihi. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyweweza kuchagua majibu sahihi kwa vipengele vyote (i - x) na kupata alama zote 10.

<b>i)</b>	C
<b>ii)</b>	D
<b>iii)</b>	C
<b>iv)</b>	E
<b>v)</b>	C
<b>vi)</b>	D
<b>vii)</b>	E
<b>viii)</b>	B
<b>ix)</b>	A
<b>x)</b>	A

Kielelezo Na. 1.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swalil*  
*la 1.*

Katika Kielelezo Na.1.1, mtahiniwa aliweza kuchagua herufi za majibu sahihi na kupata alama za juu kutokana na uelewa aliokuwa nao juu ya mada zilizotahiniwa katika swalil hili.

Hata hivyo, asilimia 27.1 ya watahiniwa waliojibu swalil hili walitoa majibu yasiyo sahihi katika vipengele vingi hivyo kupata alama hafifu kutokana na kukosa uelewa wa dhana mbalimbali zilizotahiniwa. Baadhi yao, walionesha kutokuelewa vyema matakwa ya swalil hivyo kushindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele vingi. Uchambuzi zaidi kuhusu namna watahiniwa walivyojibu swalil hili umefafanuliwa katika vipengele vya swalil hili kama ifuatavyo:

- (i) Ni neno lipi linalotoa taarifa kuhusu nomino?
- A Kitenzi
  - B Kielezi
  - C Kivumishi
  - D Kiwakilishi
  - E Kiunganishi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua dhima mbalimbali za aina za maneno katika tungo. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *C Kivumishi*, neno ambalo hufanya kazi ya kusifia au kutoa taarifa juu ya nomino au kiwakilishi. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya kivumishi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengine walikosa uelewa wa kutosha kuhusu dhima anuwai za maneno, hivyo kuchagua vipotoshi *A Kitenzi*, *B Kielezi*, *D Kiwakilishi* na *E Kiunganishi*. Uteuzi wa kipotoshi *A Kitenzi*, unaonesha kuwa watahiniwa hawakutambua kuwa kitenzi hudokeza tukio au tendo linalofanyika. Uteuzi wa kipotoshi *B Kielezi*, unatokana na watahiniwa kutokuwa na uelewa kuwa kielezi hutoa taarifa zaidi kuhusu vitenzi, vivumishi au vielezi vingine. Pia uteuzi wa kipotoshi *D Kiwakilishi*, haukuwa sahihi kwani kiwakilishi ni neno linalotumiwa/kusimama badala ya nomino. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *E Kiunganishi*, unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa kuwa ni neno au kikundi cha maneno kinachounganisha dhana mbili au zaidi.

(ii) Katika lugha ya Kiswahili kuna aina ngapi za vitenzi?

- A mbili.
- B tano.
- C sita
- D tatu.
- E nne.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za vitenzi. Watahiniwa waliojibu vizuri kipengele hiki walichagua herufi *D tatu*. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina tatu za vitenzi ambazo ni; *Vitenzi vikuu (T)*, *Vitenzi visaidizi (TS)* na *Vitenzi vishirikishi (t)*.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, C na E kutokana na kukosa uelewa juu ya dhana ya vitenzi, hivyo kushindwa

kubaini aina za vitenzi. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu idadi sahihi ya vitenzi vya Kiswahili ambavyo ni vya aina tatu yaani *kitenzi kisaidizi*, *kitenzi kikuu* na *kitenzi kishirikishi*.

(iii) Maneno yapi kati ya yafuatayo yametokana na lugha za kibantu?

- A kitindamimba na bendera
- B hela na mtutu
- C kitivo na ngeli
- D godoro na sharubati
- E bunge na shule

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika kutambua msamiazi wa Kiswahili ulioundwa kutokana na lugha za Kibantu. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *C Kitivo na ngeli* kwa sababu maneno hayo yametokana na utohoaji kutoka katika lugha za Kibantu ambapo; neno *ngeli* limetoka katika lugha ya Kihaya ikiwa na maana ya *kundi la nomino lenye sifa zinazofanana* na *kitivo* limetoka katika lugha ya Kipare/Kisambaa lenye maana ya *idara kuu ya masomo ya fani fulani*. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliokosa uelewa wa kutosha kuhusu asili ya maneno hayo na kuchagua vipotoshi A, B, D na E. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A Kitindamimba na bendera*; hawakuja kuwa asili ya neno *bendera* ni lugha ya *Kireno*. Aidha, waliochagua kipotoshi *B Hela na mtutu*, hawakuja kuwa neno *hela* lina asili ya lugha ya Kijerumani, *D Godoro na sharubati*, neno *sharubati* lina asili ya lugha ya *Kiarabu* na *E Bunge na shule*, neno *shule* linatokana na lugha ya *Kijerumani*. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi A, B, D na E ulikuwa sio sahihi kwani jozi zake zilikuwa na neno moja lisilotokana na lugha za Kibantu.

(iv) Ni mambo gani muhimu ya kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo?

- A Mada, muktadha na mazungumzo ya ana kwa ana.
- B Mada, mazungumzo na uhusiano wa wazungumzaji.

- C Mada, mzungumzaji na muktadha wa mazungumzo.
- D Mada, mzungumzaji na uhusiano wa wazungumzaji.
- E Mada, muktadha na uhusiano wa wazungumzaji.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kubaini mambo ya kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo. Watahiniwa waliokuwa na umahiri huo walichagua jibu sahihi *E Mada, muktadha na uhusiano wa wazungumzaji*.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, C na D kwa kuwa walikosa maarifa na uelewa wa kubaini mambo ya kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo. Kwa ujumla, upotoshaji uliopo katika machaguo *C* na *D* ni uwepo wa *mzungumzaji* ambaye ni mhusika katika mazungumzo na siyo jambo la kuzingatiwa katika mazungumzo. Kiuhalsia, kinachozingatiwa ni *uhusiano wa wazungumzaji* katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *A Mada, muktadha na mazungumzo ya ana kwa ana*, ilitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa mazungumzo ya ana kwa ana siyo jambo la kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo bali ni *njia ya mawasiliano*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *B Mada, mazungumzo na uhusiano wa wazungumzaji* walishindwa kuelewa kuwa *mazungumzo* siyo jambo la kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo bali ndio yanayohitaji uteuzi wa mambo hayo ili kufanikisha mazungumzo.

- (v) Bainisha kauli inayoonesha dhima muhimu za vitendawili katika jamii.
  - A Kuhimiza umoja na ushirikiano.
  - B Kupanga watu katika marika yao.
  - C Kuchochea udadisi wa mambo.
  - D Kuchochea uwongo wa mambo.
  - E Kukosoa wadadisi wa mambo.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususan mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa dhima za fasihi simulizi ili kuweza kubainisha kauli inayoonesha dhima muhimu za vitendawili katika jamii. Baadhi ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi *C Kuchochea udadisi* kwani walielewa kuwa vitendawili hujengwa kwa mafumbo yanayohitaji udadisi ili kuyafumbua.

Wapo watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, D na E kutokana na kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, uteuzi wa kipotoshi *A Kuhimiza umoja na ushirikiano*, watahiniwa walihusisha dhana ya methali (yenye dhima hiyo) na vitendawili, uteuzi wa kipotoshi *B Kupanga watu katika marika yao*, walihusisha rika kwa kufikiri kuwa vitendawili huwahu su zaidi watoto, kipotoshi *D Kuchochea uwongo wa mambo* kiliwavutia watahiniwa wengine kwa sababu walihusisha vitendawili na uongo kwa kauli zake kuficha ukweli na uteuzi wa kipotoshi *E Kukosoa wadadisi wa mambo* ulitokana na watahiniwa kukosa maarifa ya kutambua tungo za kifasihi na zisizo za kifasihi. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa kushindwa kuhusisha kauli walizopewa na dhima muhimu za vitendawili katika jamii.

- (vi) Njia mojawapo ya kuzuia utata katika lugha ya mazungumzo ni ipi kati ya zifuatazo?
- A Kuepuka makosa ya kisarufi na kimantiki.
  - B Kutumia neno lenye maana zaidi ya moja.
  - C Kutumia kiwakilishi kiambata katika neno.
  - D Kuweka msisitizo au ufanuzi zaidi.
  - E Kutumia mofimu sahihi za wakati.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha*, mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano* ambapo lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuzuia utata katika lugha ya Kiswahili. Mtahiniwa alitakiwa kubaini njia mojawapo ya kuzuia utata katika lugha ya mazungumzo kati ya njia tano alizopewa. Watahiniwa hao

waliochagua jibu sahihi *D Kuweka msisitizo au ufanuzi zaidi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia za kuzuia utata katika lugha ya mazungumzo.*

Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, C na E hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia za kuzuia utata katika lugha ya mazungumzo. Kwa mfano, uteuzi wa vipotoshi *A* *Kuepuka makosa ya kisarufi na kimantiki na E Kutumia mofimu sahihi za wakati ulitokana na watahiniwa kuchanganya njia za kuondoa utata katika sentensi na zile zinazoweza kuzuia utata katika mazungumzo. Aidha, uteuzi wa vipotoshi *B*, *Kutumia neno lenye maana zaidi ya moja* na *C*, *Kutumia kiwakilishi kiambata katika neno unaonesha kuwa*, watahiniwa hawakuja kuwa hizo ni sababu za utata katika tungo na siyo njia za kuzuia utata katika lugha ya mazungumzo kama yalivyokuwa matakwa ya swali.*

(vii) "Waandishi wa fasihi huzungumzia watu wenye mienendo isiyokubalika katika jamii ili kukemea mienendo hiyo." Katika tamthiliya ulizosoma, ni wahusika wepi kati ya wafuatao wana mienendo isiyokubalika?

- A Joti, Ngoswe na Mama Furaha.
- B Padre James, Ngoswe na Baba Anna.
- C Mazoea, Mama Furaha na Joti.
- D Ngoswe, Baba Anna na Suzi.
- E Ngoswe, Joti na Padre James.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya* ambapo lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutathmini mienendo ya wahusika katika kazi za kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini wahusika wenye mienendo isiyokubalika katika jamii. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi *E Ngoswe, Joti na Padre James*. Uchaguzi huo unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mienendo ya wahusika mbalimbali waliopo katika tamthiliya teule walizosoma. Hivyo, waliweza kuwatambua wahusika *Ngoswe, Joti*

*na Padre James* ambao mienendo yao haikubaliki katika jamii hususan katika kuchanganya mapenzi na kazi/shule.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, C na D kwa kuwa hawakuwa na uelewa kuhusu tabia mbalimbali za wahusika katika tamthiliya teule, hivyo kushindwa kuchagua jibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi *A Joti, Ngoswe na Mama Furaha, B Padre James, Ngoswe na Baba Anna, C Mazoea, Mama Furaha na Joti na D Ngoswe, Baba Anna na Suzi* ultokana na watahiniwa kukosa uelewa wa utendaji wa wahusika hao, hivyo, kutokugundua kuwa katika jozi za wahusika hao kulikuwa na wahusika waliokuwa na mienendo inayokubalika katika jamii kama vile; *Mama Furaha na Baba Anna*.

(viii) Kati ya sababu zifuatazo ni ipi **si sahihi** kuhusu matumizi ya kamusi?

- A Kujifunza lugha ya kigeni.
- B Kusanifisha maneno mapya.
- C Kubaini kategoria ya neno.
- D Kujua maana za maneno.
- E Kujua tahajia ya neno.

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno*, mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* na lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu matumizi sahihi ya kamusi. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini sababu isiyo sahihi juu ya matumizi ya kamusi kati ya sababu tano alizopewa. Watahiniwa waliokuwa mahiri katika kutumia kamusi walichagua jibu sahihi *B, Kusanifisha maneno mapya*. Watahiniwa hao, waliweza kubaini kuwa, *kusaidia kujifunza lugha ya kigeni, kubaini kategoria ya neno, kujua maana ya maneno na kujua tahajia za maneno*, zote ni sababu sahihi za kutumia kamusi.

Baadhi ya watahiniwa walichagua vipotoshi *A Kujifunza lugha ya kigeni, C Kubaini kategoria ya neno, D Kujua maana za maneno na E Kujua tahajia ya neno*, kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya sababu za matumizi ya kamusi. Hivyo, kushindwa kutambua

sababu **isiyo** sahihi kuhusu matumizi ya kamusi. Kimsingi, watahiniwa hao walichagua vipotoshi ambavyo vyote ni sababu sahihi kuhusu matumizi ya kamusi kwani dhima za kutumia kamusi ni pamoja na kusaidia kujifunza lugha ya kigeni, kubaini kategoria ya neno, kujua maana ya maneno na kujua tahajia za maneno.

- (ix) Ni methali ipi **inayokinzana** na methali “Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu?”
- A Manahodha wengi, chombo huenda mrama.
  - B Palipo na wengi, hapaharibiki neno.
  - C Haba na haba, hujaza kibaba.
  - D Kidole kimoja, hakivunji chawa.
  - E Fimbo ya mnyonge, ni umoja.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi* na lilenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika kubaini maana zinazodhahirika katika methali. Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua methali inayokinzana na methali “*Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu*” kati ya methali tano alizopewa. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *A Manahodha wengi, chombo huenda mrama*. Watahiniwa hao, walikuwa na uwezo wa kutambua maana za methali katika pande mbili za fikra ambazo huashiria tendo hivyo kuweza kutambua methali inayokinzana na methali “*Umoja ni nguvu utengeno ni udhaifu*”.


Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi *B Palipo na wengi, hapaharibiki neno, C Haba na haba, hujaza kibaba, D Kidole kimoja, hakivunji chawa* na *E Fimbo ya mnyonge, ni umoja*. Watahiniwa hao, hawakujua maana ya methali “*Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu*” hivyo kushindwa kubaini methali inayokinzana na methali hiyo kuwa ni *Manahodha wengi, chombo huenda mrama*. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi B, C, D na E ambavyo kimsingi vilibeba methali zinazofanana kimaana na methali “*Umoja ni nguvu utengeno ni udhaifu*”.

- (x) Bainisha sentensi ambatano yenyé muundo wa sentensi changamano mbili kati ya sentensi zifuatazo:
- A Gari lililomteka tumeliona na dereva aliyetekwa ameonekana.
  - B Mtoto aliyeumia jana amelazwa na mtoto mwingine hajitambui.
  - C Mpe haki yake yote ili nae akupe haki yako yote.
  - D Uchaguzi uliofanyika juzi umezaa matunda.
  - E Baba anataka kujenga nyumba lakini mama hataki kabisa.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mjengo wa Tungo* hususan mada ndogo ya *Aina za Tungo* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa kuhusu muundo wa sentensi ambatano. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *A Gari lililomteka tumeliona na dereva aliyetekwa ameonekana*. Watahiniwa hao, waliweza kubaini kuwa sentensi hiyo ni sentensi ambatano iliyoundwa na sentensi changamano mbili ambazo ni; "Gari lililomteka tumeliona" na "Dereva aliyetekwa ameonekana." Aidha, sentensi hizo zimeunganishwa na kiunganishi "na". Hivyo, watahiniwa wa kundi hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya miundo ya sentensi ambatano kiasi cha kuweza kuchagua herufi yenyé jibu sahihi.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi *B, C, D* na *E* kutokana na kukosa uelewa juu ya miundo ya sentensi ambatano. Kwa mfano, watahiniwa waliochagua kipotoshi *B Mtoto aliyeumia jana amelazwa na mtoto mwingine hajitambui* walishindwa kuelewa kuwa, sentensi ya pili katika sentensi hiyo *Mtoto mwingine hajitambui* si sentensi changamano bali ni sentensi sahihi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *C Mpe haki yake yote ili nae akupe haki yako yote*, hawakuelewa kuwa sentensi hii ni ambatano lakini yenyé muundo wa sentensi sahili mbili na sio sentensi changamano mbili kama yalivyokuwa matakwa ya swalí. Pia, waliochagua kipotoshi *D Uchaguzi uliofanyika juzi umezaa matunda* hawakuelewa kuwa ni sentensi changamano (moja) na kipotoshi *E Baba anataka kujenga nyumba lakini mama hataki*, sentensi ya pili katika sentensi hiyo ni sentensi sahili na sio changamano kinyume na matakwa ya swalí.

Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuzingatia kuwa, swali hilo lilimtaka mtahiniwa kubainisha sentensi ambatano yenyeye muundo wa sentensi mbili ambazo ni *changamano*. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuchagua jibu sahihi katika vipengele vyote hivyo, kupata alama hafifu.



Kielelezo Na. 1.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.*

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kipengele hata kimoja na kupata 0 kutokana na kukosa maarifa kuhusu dhana mbalimbali katika mada zilizotahiniwa katika kipengele cha (i) hadi (x).

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha


Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera* vya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Swali liliuliza;

*Oanisha maana za vipera vya Fasihi Simulizi katika Safu A na dhana za Fasihi Simulizi zilizo katika Safu B; kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.*

<i>Safu A</i>	<i>Safu B</i>
(i) <i>Sherehe au shughuli zinazofanyanya na jamii katika kipindi maalum cha mwaka.</i>	A <i>Utani</i>
(ii) <i>Masimulizi ya mambo ya kishujaa ambayo mtu amewahi kuyafanya maishani mwake.</i>	B <i>Matambiko</i>
(iii) <i>Maigizo mafupi yaliyojaa ucheshi na mzaha.</i>	C <i>Miviga</i>
(iv) <i>Sadaka itolewayo kwa miungu au mahoka.</i>	D <i>Harusi</i>
(v) <i>Masihara wanayofanyiana wanajamii wakati wa shida na raha.</i>	E <i>Ngoma</i>
	F <i>Majigambo</i>
	G <i>Vichekesho</i>

Swali lilikuwa na jumla ya vipengele vitano ambapo mtahiniwa alitakiwa kuoanisha maana za vipera vyta fasihi simulizi vilivyokuwa katika safu A na dhana zake katika safu B. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Watahiniwa 435,082 sawa na asilimia 99.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 403,895 sawa asilimia 92.8 walifaalu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 2 inaonesha viwango vyta ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 2:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2

Katika Chati Na. 2, watahiniwa 31,187 (7.2%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1, watahiniwa 178,239 (40.9%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 1.5 hadi 3 na watahiniwa 225,656 (51.9%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi alama 5.

Asilimia 51.9 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Watahiniwa hao waliweza kuoanisha kwa usahihi maana za vipera vya fasihi simulizi zilizokuwa katika Safu A na dhana za fasihi simulizi katika Safu B kwa kuandika; (i) *C Miviga*, (ii) *F Majigambo*, (iii) *G Vichekesho*, (iv) *B Matambiko na* (v) *A Utani*. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swalii hili na kupata alama za juu.

02.	i) C
	ii) F
	iii) G
	iv) B
	v) A

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swalii la 2.*

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeweza kuoanisha kwa usahihi maana ya vipera vya fasihi simulizi katika Safu A na dhana za fasihi simulizi zilizo katika Safu B kwa kuandika herufi sahihi zenye dhana zinazowiana na maana za vipera vya fasihi simulizi (i - v).

Aidha, asilimia 40.9 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walionesha kuwa na maarifa ya wastani kuhusu maana ya vipera vya fasihi simulizi hivyo kushindwa kutambua baadhi ya dhana zinazowakilisha maana za vipera vya fasihi simulizi na kufaulu

kwa kiwango cha wastani. Kwa ujumla, majibu ya watahiniwa hao hayakuwa sahihi kwa baadhi ya vipengele.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana (7.2%) ndio walioonesha kushindwa kuoanisha maana za vipera vya fasihi simulizi zilizokuwa katika safu A na dhana husika katika Safu B kwa kiasi kikubwa. Baadhi yao, walichagua vipotoshi *D Harusi* na *E Ngoma* dhana ambazo hazihusiani na maana zote zilizopo katika safu A. Hii ilitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa juu ya maana ya vipera vya fasihi fimulizi. Vilevile, watahiniwa hao walifikiri kuwa, sherehe au shughuli zinazofanywa na jamii katika kipindi maalum cha mwaka *ni harusi* kutokana na maono yao kuwa, harusi nyingi hufanywa mwishoni mwa mwaka badala ya kubaini dhana sahihi inayobebwa na maana hiyo kuwa ni *miviga*. Pia watahiniwa wengine katika kuoanisha maana ya kipengele (iii) walichagua kipotoshi A *Utani* kwa kukosa maarifa na kuona kuwa maigizo mafupi yaliyojaa ucheshi na mzaha ni *utani* badala ya *vichekesho*. Kielelezo Na. 2.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi maana za vipera vya fasihi simulizi na dhana za Fasihi Simulizi na kupata alama hafifu.

2:	D
	G
	A
	C
	B

Kielelezo Na. 2.2: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swalii la 2.*


## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali sita (6) yanayohitaji majibu mafupi na ilikuwa na jumla ya alama 40. Sehemu hii ilihu mada ya *Aina za Maneno, Matumizi ya Lughu, Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi (Uhakiki wa Riwaya), Uhakiki wa kazi za Fasihi Simulizi na Uandishi*.

### **2.2.1 Swali la 3: Aina za Maneno**

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno*, mada ndogo ya *Ubainishaji wa Aina za Maneno* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa aina za maneno. Swali lilitaka mtahiniwa kuainisha maneno yaliyokolezwa wino katika tungo alizopewa ambapo lilikuwa na jumla ya alama nne (4).

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 394,750 sawa na asilimia 90.2 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Kiwango cha ufaulu wa swali hili ni cha wastani kwani watahiniwa 178,555 sawa na asilimia 45.2 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 3:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3

Katika Chati Na. 3, watahiniwa 216,195 (54.8%) walifaalu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1, watahiniwa 58,798 (14.9%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 1.5 hadi 2.5 na watahiniwa 119,757 (30.3%) walifaalu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa (54.8%) walishindwa kuainisha kwa usahihi maneno yaliyokolezwa wino kutoekana na kuwa na

uelewa mdogo juu ya aina za maneno. Mionganini mwao, watahiniwa 149,225 sawa na asilimia 37.8 walishindwa kuanisha neno hata moja na kupata 0. Kati ya watahiniwa hao, wapo walioshindwa kuelewa matakwa ya swali na kuandika upya maneno yaliyokolezwa wino badala ya kuainisha maneno hayo kama ilivyotakiwa. Aidha, wengine hawakuelewa matakwa ya swali kutokana na kutokuelewa kuwa neno "ainisha" lina maana ya kubaini aina ya neno lililokolezwa wino. Watahiniwa hao, walijibu kwa kutaja *nafsi ya kwanza*, *pili na tatu* kutoka katika maneno waliyopewa kutokana na uelewa mdogo kuhusu aina za maneno.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walainisha maneno yasiyo sahihi kulingana na maelekezo ya swali kwa kuorodhesha baadhi ya maneno yaliyokuwa katika sentensi (i - iv). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibaini vitenzi au viwakilishi vilivyokuwa katika sentensi hizo kama vile; (i) *waliondoka*, (ii) *watashiriki*, (iii) *niwaeleze* na (iv) *wawakilishi* kinyume cha matakwa ya swali. Kielelezo Na. 3.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuainisha maneno yaliyokolezwa wino katika tungo walizopewa.

3. (i) Tungo Sentensi
(ii) Tungo kishazi
(iii) Tungo kirai
(iv) Tungo neno

Kielelezo Na. 3.1: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swali la 3.*

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa aliandika aina za tungo katika vipengele (i) hadi (iv) kinyume na matakwa ya swali ambapo alipaswa kuainisha maneno yaliyokolezwa wino. Mtahiniwa huyo alijibu kama ifuatavyo; (i) *Tungo sentensi* badala ya kiwakilishi, (ii) *Tungo kishazi* badala ya kivumishi, (iii) *Tungo kirai* badala ya kielezi na (iv) *Tungo neno* badala ya *kitenzi*. Hata hivyo,

mtahiniwa huyo alionesha kutokuwa na maarifa kuhusu aina za tungo kwa kuandika *tungo neno* ambayo kiuhalisia haipo.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa (30.3%) walimudu kujibu swalii hili vizuri kutoptaka na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno. Watahiniwa hao, waliweza kuainisha maneno yaliyokolezwa wino katika tungo walizopewa katika vipengele vyote (i - iv). Kwa ujumla, walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana hizo kuwa; (i) neno "wangapi" ni kiwakilishi kwani limetumika kuwakilisha nomino. (ii) Neno "wangapi" limetumika kama kivumishi kwa kuwa linaelezea zaidi juu ya nomino *wachezaji*, (iii) neno "mara ngapi" limetumika kama kielezi kwani linaelezea zaidi kuhusu kitenzi *niwaeleze* na (iv) neno "waliunga" ni kitenzi kwani kimetaja kitendo kilichofanywa na *wawakilishi* wote. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swalii hili na kupata alama za juu.

3.	
i.	Wangapi - ni Kiwakilishi
ii.	Wangapi - ni Kivumishi
iii.	Mara ngapi - ni Mielezi
iv.	Waliunga - ni Mitenzi

Kielelezo Na. 3.2: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swalii la 3*


Kielelezo 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeainisha kwa usahihi maneno yaliyokolezwa wino katika tungo alizopewa na kupata alama zote.

Aidha, asilimia 14.9 ya watahiniwa waliweza kuainisha baadhi ya maneno yaliyokolezwa wino na kushindwa maneno mengine hivyo kuwa na ufaulu wa wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliainisha maneno katika vipengele (i) na (iv) kwa usahihi na kushindwa maneno yaliyokuwa katika vipengele (ii - iii) kwa kuandika *kiwakilishi* na *kivumishi* mtawalia badala ya (ii) kivumishi na (iii) kielezi hivyo kupata alama za wastani.

## 2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Aina za Maneno* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kufafanua aina za maneno. Swali limtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi mazingira manne ambayo kielezi huweza kujipambanua, kisha kutunga sentensi moja kwa kila aina ya mazingira. Swali likuwa na jumla ya alama 4.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 360,356 sawa na asilimia 82.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Hili ni swali lililojibiwa na idadi ndogo zaidi ya watahiniwa ikilinganishwa na maswali mengine ya lazima. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 121,138 sawa na asilimia 33.6 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 4:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4

Katika Chati Na. 4, watahiniwa 239,218 (66.4%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1, watahiniwa 48,186 (13.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 1.5 hadi 2.5 na watahiniwa 72,952 (20.2%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 66.4 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walikuwa na ufaulu hafifu kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya mazingira ambayo kielezi huweza kujipambanua. Baadhi yao, katika kundi hili waliweza kubaini kuwa mazingira yanayopambanua kielezi ni *mahali* pekee na kushindwa kubaini mazingira mengine hivyo kupata alama hafifu. Watahiniwa wengine (165,657) sawa na asilimia 46.0 walipata alama 0 kutokana na kushindwa kubaini mazingira hata ya aina moja ambayo kielezi huweza kujipambanua. Baadhi ya watahiniwa walielezea mazingira ya kawaida kama vile; *shuleni, hospitalini* na *mazingira mengine kama hayo* badala ya kueleza kwa ufupi mazingira manne ambayo ni; *mahali, idadi, wakati na namna/jinsi*. Hata hivyo, watahiniwa hao walishindwa kutunga sentensi sahihi kwa kila aina ya mazingira. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kushindwa kukidhi matakwa ya swalii.

4. ↗ Shuleni	
mpano kaka amoendo shuleni	E
↗ Huuooa kusimama kidosi no kitenai	
mpano Amolima too basubushi	E
↗ Huuooa kusimama kidosi no kicankishu	
mpano Sini talkuu dukani	E
↗ Huuooa kusimama no kiwimishi	
mpano Binti mrefu yupo sokoni	E

Kielelezo Na. 4.1: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swalii la 4.*

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alishindwa kueleza kwa ufupi mazingira manne ambayo kielezi huweza kujipambanua badala yake alielezza miundo ya vielezi na kutunga sentensi zisizokidhi matakwa ya swalii.

Watahiniwa wachache walioweza kujibu swalii hili vizuri walikuwa 72,952 sawa na asilimia 20.2. Watahiniwa hao, walionesha kuwa na uelewa mkubwa kuhusu mazingira ambayo kielezi huweza kujipambanua pamoja na kutunga sentensi moja kwa kila aina ya mazingira kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza vizuri kwa kubaini aina za vielezi kama vile; (i) kielezi cha mahali: hueleza sehemu tendo linapofanyika, mfano *kaka anacheza uwanjani*, (ii) kielezi cha idadi: hufafanua mara ngapi tendo limetendeka, mfano *Joeli ameshinda mara mbili*, (iii) kielezi cha wakati: hueleza lini tendo limetendeka, mfano *Shangazi alikuja mwaka jana* na (iv) kielezi cha namna/ jinsi: hueleza ni vipi tendo linavyofanyika, mfano *Joshua anacheza polepole*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi swalii hili.

4. Aina za kielezi
i) Kielezi cha namna : Hibi hueleza jinsi ambayo tende limefanyika. mfano; Aina anatembea taratibu E
ii) Kielezi cha wakati ; Hibi hueleza tende limefanyika muda gani mfano; Aina aliendoka alifayiri. E
iii) Kielezi cha matali ; Hibi ni kielai kinachotoa taarifa kuhusu matali jumbo Umepeonyiba mfano; mitoto amelala kitarekani. E
iv) Kielezi cha idadi; Hibi hueleza jumbo Umepeonyika mara recipi mfano; Mwemangu nimechukanya mara nyangi latini kutabu tunelewa E

Kielelezo Na. 4.2: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swalii la 4.*


Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa aliweza kueleza kwa ufupi mazingira manne yanayopambanua vielezi kama vile; *namna/jinsi, wakati/muda, sehemu/mahali* na *kiasi/idadi*, kisha kutunga sentensi moja kwa kila aina ya mazingira.

### 2.2.3 Swalii la 5: Matumizi ya Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha* katika *Miktadha Mbalimbali* na mada ndogo ya *Utata* katika *Mawasiliano*. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuzongoa utata katika tungo. Swali likuwa na jumla ya alama (8) na lilimtaka mtahiniwa kueleza maana mbili kwa kila tungo zifuatazo:

- (a) *Mama anaota.*
- (b) *Tafadhali nipe sahani ya kulia.*
- (c) *Vijakazi wanalima barabara.*
- (d) *Amekanyaga mtoto.*

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 428,551 sawa na asilimia 97.9 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 386,391 sawa asilimia 90.2 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 5:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swalii la la 5

Katika Chati Na. 5, watahiniwa 42,160 (9.8%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2, watahiniwa 171,618 (40.1%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 214,773 (50.1%)

walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8.

Asilimia 50.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu vizuri kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya tungo zenye maana zaidi ya moja. Watahiniwa hao, waliweza kueleza maana mbili kwa kila tungo walizopewa kama vile; (a) (i) kupata joto la juu (ii) kupata njozi; (b) (i) chombo cha kuwekea chakula (ii) chombo kilichopo upande wa kulia, (c) (i) vijakazi wanalima vizuri (ii) vijakazi wanalima njia na (d) (i) mtoto amekanyagwa (ii) mtoto amekanyaga kitu fulani. Kielelezo Na. 5.1 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

S.	(a) - Mama anaona njozi aktiba amelala. - Mama amekau Karibu na moto.
	(b) - Sahani iliyoko upande wa Kulia. - Sahani Kwa ajili ya Kula Chakula.
	(c) - sawasawa. - nji umbayo watu hupita.
	(d) - Mtoto amekanyaga sehemu/mahali. - Mtu amekanyaga mtoto.

Kielelezo Na. 5.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali la 5.*

Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeleza kwa usahihi maana mbili kwa kila tungo alizopewa na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 40.1 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kueleza baadhi ya maana zisizojitosheleza kwa kila tungo walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana moja inayodhahirika kwa kila tungo lakini alishindwa kueleza maana ya

pili iliyopo katika tungo husika (a) - (d) hivyo akapata alama za wastani.

Licha ya ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swalii hili, watahiniwa wachache sawa na asilimia 9.8 walionesha kuwa na uelewa mdogo juu ya tungo zenyé maana zaidi ya moja walizopewa. Watahiniwa hao, walishindwa kueleza maana mbili kwa kila tungo walizopewa kwenye kipengele (a) hadi (d) hivyo kupata alama hafifu. Baadhi yao, walionesha kutokulielewa swalii vyema hivyo kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swalii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga sentensi zinazoelekea kukanusha tungo alizopewa ambapo aliandika katika kipengele (a) *Mama haoti*, (b) *Tafadhali usinipe sahani ya kulia*, (c) *Vijakazi hawalimi barabara na* (d) *Hajakanyaga mtoto* badala ya kueleza maana mbili zilizopo katika kila tungo kama vile; (a) (i) kupata joto la jua (ii) kupata njozi; (b) (i) chombo cha kuwekea chakula (ii) chombo kilichopo upande wa kulia; (c) (i) vijakazi wanalima vizuri (ii) vijakazi wanalima njia na (d) (i) mtoto amekanyagwa (ii) mtoto amekanyaga kitu fulani. Aidha, wapo watahiniwa walibainisha ngeli mbalimbali za nomino na wengine walibainisha aina za maneno katika tungo hizo kutokana na kutokuelewa matakwa ya swalii. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kushindwa kukidhi matakwa ya swalii.

5.	(a) Mama 'anoda
	→ Hii inonyesha hali ya umoja katika ngeli ya A-WA
	→ Hii ina'kishazi huru
(b)	Tafadhali nipe sahani ya kaulia
	→ Hii inonyesha Haliya umoja katika ngeli ya YA-ZA
	→ Hii ni kishazi huru
(c)	Vijakari wanalima barabara
	→ Hii ina onyesha eti Hali ya wingi katika ngeli ya A-WA
	→ Hii ni kishazi huru
(d)	Ampakanyaga mtoto
	→ Hii khonyesha hali ya kutenda.
	→ Hii inonyesha Hali ya umoja. Katika ngeli ya A-WA

Kielelezo Na. 5.2: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swalii la 5.*

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alishindwa kueleza maana mbili kwa kila tungo alizopewa badala yake alitaja *hali ya umoja na wingi, ngeli, kishazi na kauli ya kutenda* katika majibu yake.

#### 2.2.4 Swalii la 6: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya*. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutathmini kazi za kifasihi. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi madhara manne yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemavu wa ngozi kwa kutumia mifano kutoka

katika riwaya ya Takadini. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama (8).

Watahiniwa 408,889 sawa na asilimia 93.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 346,079 (84.6%) walifaalu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

### **Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya Wanafunzi
0.0 - 2.0	171,596	15.4
2.5 - 5.0	143,988	35.2
5.5 - 8	202,091	49.4

Katika Jedwali Na. 2, watahiniwa 171,596 (15.4%) walifaalu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2, watahiniwa 143,988 (35.2%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 202,091 (49.4%) walifaalu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8.

Karibu nusu ya watahiniwa (49.4%) walifaalu kwa kiwango cha juu kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha ya kuchambua maudhui katika kazi za fasihi hususan riwaya teule. Aidha, watahiniwa hao waliweza kutumia mifano sahihi kutoka katika riwaya ya “Takadini” kueleza madhara manne yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemavu wa ngozi. Walitoa hoja sahihi kama vile; (i) *kuendelea kuuwawa kwa walemavu wa ngozi*, (ii) *husababisha mifarakano katika jamii*, (iii) *kusababisha vita na visasi katika jamii* na (iv) *kusababisha hofu katika jamii au umaskini katika jamii*. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

6. Madhara yanayoweza kutokea.

i/ Familia kusambaratika. Hii inaonekana pale ambapo sekai anamua kutooka na mtoto wake Takadini kwa lengo li kuokoa maisha ya mtoto wake. Na hivyo baci kuorhona na mume wake Makwati na hivyo wan kutengana kama familia yoani mume kubaki peke yake na mke kubaki peke yake na mtoto.

ii/ Kuzidisha idadi ya vifo kuwenye jamii. Hii inaonekana pale kuwenye kijiji cha Mtemi Zvedi ambapo uanamua sekai pamoja na mtoto wake wote unuuwe kutoka na kufuateli milla potofu ya kuwabagua walemaru wa ngozi.

iii/ Kupunguza nguvu kazi ya wanajamii katika jamii husika. Hii inaonekana kupitia sekai ambapo baada ya kuona kwamba milla potofu za kuwabagua walemaru wa ngozi katika kijiji cha Mtemi Zvedi zimepambaa moto na hivyo kuamua kukimbia na kwenda katika kijiji kingine. Lakini pia kuwanjima haki za za msingi. Hii ni kutohara na jinsi Nhamo aliyekuwa anamnyanyawa Takadini kutohara na kuhisi anamuibia mpenzi wake.

iv/ Helela mifarakano na migogoro katika jamii yetu. Hii ni kutohara na Makwadi baada ya kuona sekai mke ambaye atiampenda sana amemzalia upere na hivyo kumtubumu sekai kutohara muaminifu kunko pia huenda atakuwa amelaaniwa.

Kielelezo Na. 6.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali la 6.*

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi madhara manne yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemaru wa ngozi kama vile; kuwapo kwa matabaka, migogoro, kusambaratika kwa familia na kupoteza nguvu kazi ya jamii. Vilevile, alitumia mifano sahihi kutoka katika riwaya ya Takadini.

Kwa upande mwingine, asilimia 35.2 ya watahiniwa walijibu swalii hili na kupata alama za wastani. Ufaulu huo ulitokana na kumudu kufafanua madhara machache yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemvu wa ngozi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja mbili sahihi ambazo ni; *kuongezeka kwa hofu na kufarakana kwa jamii*, lakini alitoa hoja nyingine mbili zisizo sahihi kwa kuandika; *italeta utajiri kwa jamii* na *idadi ya walemvu wa ngozi itapungua*, madhara ambayo hayakulengwa na mwandishi wa riwaya hiyo.

Watahiniwa wachache (15.4%) walijibu vibaya swalii hili na kupata alama hafifu kutokana na kukosa uelewa kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi andishi hususan riwaya ya “Takadini” inayozungumzia ulemavu wa ngozi au albino. Watahiniwa hao walionesha kushindwa kutumia mifano kutoka katika riwaya hiyo ili kueleza kwa ufupi madhara manne yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemvu wa ngozi. Baadhi yao, walijadili dhamira mbalimbali zilizopo katika riwaya ya “Takadini.” Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja kama vile; *mapenzi na ndoa, mila na desturi, ndoa za mitala* na nyingine zisizoendana na matakwa ya swalii. Aidha, mtahiniwa mwingine alielezea wasifu wa wahusika katika riwaya hiyo kama vile *Makwati (muumini wa ndoa za mitala, Sekai (mwathirika wa kuzaa albino)*, *Takadini (mtoto sope aliyetakiwa kuuawa)* na wahusika wengine badala ya kueleza madhara manne yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemvu wa ngozi kama vile; *jamii kuwa na mafarakano, vita/visasi, hofu, kukosa maendeleo na familia kutengana*. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swalii hili na kupata alama hafifu.

i / Kuwepo kwa mila potofu, pale fakadini alipocamu liwa na wana kijiji kutoka kuwawa kwamba amezaluu Sipe (zenzenu)
ii / Mila na desturi, kwamba wanajamii walipo sema "Kutoka famaduni yetu haini hivyo mto mwenye utemavu wa ngozi kishii na hata mapache warili mmoja uzima auwae.
iii / Suala unyanyesaji - kwani wanajamii walianiu kwamba fakadini hali wege kusoga mto mwenye rangi sawa na uengine upokiona yeyehi.

Kielelezo Na.6.1: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swali la 6.*

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alijadili dhamira mbalimbali kama vile; *uwepo wa mila potofu, mila na desturi na unyanyasaji* badala ya madhara yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu ya kuwabagua walemvu wa ngozi hivyo kupata alama hafifu katika swali hili.

## 2.2.5 Swali la 7: Uhakiki wa Ushairi


Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi* na lilenga kupima uwezo wa mtahiniwa kuchambua maandishi ya kifasihi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 8 na lilimtaka mtahiniwa kusoma shairi lifuatato kisha kujibu maswali yaliyofuata;

*Chawa huyo ni kinyozi, mtia wembe kichwani,  
Ndiye huharibu ngozi, anapokata fashini,  
Chawa ni huyo mkazi, uliyenaye jirani,  
Usimdhanie mbuzi, huyo yuko majanini,  
Wala usidhani funzi, umuonaye shambani,  
Hawa hawana ujuzi, wa kukunyoa mtani,  
Panapouma ufizi, sumu hutoka kinywani,  
Wapi hutokea nzi, kama si pako chooni,  
Chawa aliye kichwani, ni huyo kinyozi wako.*

*Chawa unapomuona, upesi muweke dole,  
 Usimwache kunona, mpaka uzue kelele,  
 Jitahidi kumbana, akatokomee mbele,  
 Ukimwacha kutuna, atakutia upele,  
 Usije kula dona, na kutafuta mchele,  
 Chawa usimpe jina, abaki akutawale,  
 Ukianza kujikuna, mtafute kwenye nywele,  
 Na nguoni hujibana, mkame kama nyenyele,  
 Chawa aliye kichwani, ni huyo kinyozi wako.*

Swali hili lilimtaka mtahiniwa katika vipengele (a) kutoa hoja mbili zinazofafanua mtindo uliotumika katika shairi hilo, (b) kueleza maana ya msemo alioutumia mwandishi "Chawa unapomuona upesi muweke dole", (c) kueleza mtazamo wa mtunzi wa shairi, (d) (i) kuandika methali moja inayosadifu shairi hilo na (ii) kueleza jinsi shairi hilo linavyoendana na maisha halisi ya jamii zetu.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 379,468 sawa na asilimia 86.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili liliwa na ufaulu wa wastani ambapo watahiniwa (168,086) sawa na asilimia 44.3 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 6:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la la 7

Katika Chati Na. 6, watahiniwa 211,382 (55.7%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2, watahiniwa 125,534 (33.1%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 42,552 (11.2%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8.

Zaidi ya nusu ya watahiniwa (55.7%) walijibu swalii hili na kupata alama hafifu kutokana na kushindwa kutoa majibu katika vipengele vingi. Kwa mfano, katika kipengele (a) baadhi yao walifafanua mtindo wa shairi kwa namna tofauti. Mtahiniwa mmoja alieleza kuwa ni mtindo *usiokuwa na vina, mizani na idadi sahihi ya mistari* na mwingine aliandika kuwa, mtindo wa shairi ni *masimulizi ya kinyozi na chawa kinyume* cha uhalisia wa shairi hilo la kimapokeo ambalo limezingatia urari wa vina, mizani na idadi ya mistari kumi kwa kila ubeti. Katika kipengele (b) walishindwa kueleza maana ya msemo uliotumika kwa kutoa hoja zisizo sahihi ambapo baadhi yao waliandika, *mbanie katikati ya vidole gumba* na wengine wakaandika, *muweke katikati ya mkono ili asikimbie* na *muue kwa vidole* badala ya kueleza udhibiti wa mapema wa mwenendo usio mzuri wa watu walio karibu nasi ili kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa nao.

Katika kipengele (c), baadhi walieleza mtazamo wa mwandishi kwa kutoa hoja zisizo sahihi kulingana na kifungu cha ushairi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *ni mtu mwenye majungu, mfitini na mwenye kutumia lugha ya matusi* na mwingine aliandika kuwa mtunzi wa shairi hili ni *msafi na anayewachukia chawa* badala ya kueleza mtazamo wa mtunzi amba ni kuitaka jamii kuchukua tahadhari mapema ili kukwepa matatizo yanayoweza kusababishwa na watu wa karibu wanaoishi nao. Aidha, katika kipengele (d) (i) baadhi, walinakili msemo uliotumika katika shairi "*Chawa unapomuona upesi muweke dole*" na wengine waliandika *methali mseto* zisizokuwa na uhusiano wowote na kifungu cha ushairi badala ya kuandika methali mojawapo kati ya zifuatazo: "kikulacho ki nguoni mwako/akumulikaye mchana usiku atakuchoma/mdharau mwiba mguu huota tende."

Pia, katika kipengele (d)(ii) baadhi waliandika juu ya *usafi wa mwili na mazingira* mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *chawa husababishwa na uchafu, jamii haipaswi kuwa na chawa* na wengine waliandika kuhusu *madhara ya chawa* katika *mwili wa binadamu* ambapo mmoja wao aliandika *chawa huaribu ngozi na kutia upele* badala ya kueleza uhalsia kuwa matatizo mengi yanayotokea katika *jamii husababishwa* na watu wa karibu wa wahanga husika. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kipengele hata kimoja na kupata 0.

7.1/ shauri hili limetumika kama Majigambo.
"shauri hili limetumika kama Ngonjera."
b/ kidole kimoja hakivunji chawa.
c/ Mtazamo wa shauri hili mtazamo wake kinyozi hajinyo'i na mganga auwezi kuji' gango.
d/ i/ Kidole kimoja hakivunji chawa. ii/ Tuzikate tamaa ya-maisha tusinge mbele na tuzidi kusambana kuwa namna moja ama nyingine kikupata mambo chanya.

Kielelezo Na. 7.1: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swali la 7.*

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alitoa majibu yasiyozingatia matakwa ya swali katika vipengele vyote vya swali hili kwa kuandika mtindo wa shairi ni *majigambo na ngonjera* katika kipengele (a); katika (b) na (d) aliandika methali isiyo na uhusiano na kifungu cha ushairi kama "kidole kimoja hakivunji chawa" na kuandika mtazamo wa mtunzi katika (c) kuwa ni *kinyozi hajinyo'i* na *mganga hajigangi* kinyume na uhalsia unaodhihirika katika kifungu cha ushairi.

Pamoja na ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kuwa wa chini, watahiniwa wachache sawa na asilimia 11.2 walifaalu kwa

kiwango kizuri kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi simulizi hususan ushairi hivyo kuweza kujibu kwa usahihi maswali katika vipengele vingi vya swali hili. Katika kipengele (a) walifanua mtindo sahihi wa shairi hilo ambalo ni *la kimapokeo lilitlozingatia urari wa vina, mizani na idadi ya mistari kumi kwa kila ubeti*. Katika kipengele (b) walieleza maana ya msemo wa mwandishi "Chawa unapomuona upesi muweke dole" *kuwa ni udhibiti wa mapema wa mwenendo usio mzuri wa majirani ili kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa nao*. Aidha, katika kipengele (c) walieleza mtazamo wa mwandishi kuwa ni *kuchukua tahadhari mapema ili kukwepa matatizo yanayoweza kusababishwa na watu wa karibu tunaoishi nao*. Vivyo hivyo, katika kipengele (d) (i) waliweza kuandika methali zinazosadifu shairi hilo kati ya hizi; *kikulacho ki nguoni mwako, akumulikaye mchana usiku atakuchoma na mdharau mwiba mguu huota tende* kama iliviyotakiwa. Katika kipengele (d) (ii) walieleza uhalsia wa shairi hilo kuwa matatizo mengi yanayotokea katika jamii husababishwa na watu wa karibu tunaoishi nao. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

<p>7. a) Mtindo uliotumika ni mtindo wa kimapokeo. Hii ni kwa rasabu ya;</p> <p>(i) Uwezo wa kituo baki arbahe kinayaran kwa beti zote</p> <p>(ii) Urari wa vina na mizani katika shairi yaani kila beti lira mifororo yenye mizani 16 kila nneja na vina nya kati na nya muisiko vinavyopandana (vinavyoparava)</p> <p>b) Mwandishi anaanaishia pale unapomuora au kungundua ntu muone kuvoko mchukulie hatua karaka (upesi) na wala ulivunishie nane wake arba unauza kuleta madhara makubwa.</p>
---

7.	<p>c) Mtazamo wa mtunzi wa shairi hili ni kwanzaa mti wa karibu ndye nusenye. Kuwa wa kikulacho madhara makubwa kwa kuwa yeye ndye yupo jirani na wewe na hiiyo unapogundua kuwa mti wa karibu si mwenya kusoko basi unapanya kumchukula hatua uperi.</p> <p>d) i) Kikulacho Kinguni mwako.</p> <p>(ii) Shairi hili linajenda na jarni yetu kwa kien kikubwa kwa sababu katika jarni yetu watu wa karibu fiaa ndio wanawababiha alihisi na madhara makubwa kwenet kwa kuwa wanatuyahana hivyo wengi waso huchukua nafasi hiyo kutekandaniwa kwa kintendwa Ubaya kwa nafasi ndugu watu wengi kuseye jarni yetu wara tabia hiyo</p>
----	---

Kielelezo Na.7.2: Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote (a - d) vilivytokana na ubeti wa ushairi.


Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa (33.1%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele (c) na (d) kwa kuandika; (c) mtazamo wa mtunzi wa shairi si wa kizalendo badala ya mzalendo na mtoa tahadhari na (d) aliandika methali inayosadifu shairi hili kuwa ni *mvumilivu hula mbivu* badala ya *kikulacho ki nguoni mwako/akumulikaye mchana usiku atakuchoma/mdharau mwiba mguu huota tende* hivyo kupata alama za wastani.

### 2.2.7 Swali la 8: Uandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Uandishi wa Barua/Matangazo*. Swali hili lililenga kupima umahiri wa

mtahiniwa katika kuunda matangazo mbalimbali. Swali lilimtaka mtahiniwa katika kipengele (a) kueleza kwa kifupi tofauti ya msingi kati ya barua ya mwaliko na tangazo na katika kipengele (b) kuandika tangazo la kumtafuta ndugu yake wa kiume anayeitwa Masana Madale aliyepotea. Swali lilikuwa na jumla ya alama 8.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 429,434 sawa na asilimia 98.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Hili ni swali lililojibiwa vizuri zaidi na watahiniwa wengi. Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, asilimia 94.8 walifaalu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 7:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8

Katika Chati Na. 7, watahiniwa 22,394 (5.2%) walifaalu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2, watahiniwa 228,788 (53.3%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 178,252 (41.5%) walifaalu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8.

Asilimia 41.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaalu kwa kiwango kizuri ambapo asilimia 4.5 walifaalu vizuri zaidi na kupata alama zote 8. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa kifupi

tofauti ya msingi kati ya barua ya mwaliko na tangazo kuwa; barua ya mwaliko ni *taarifa ya maandishi anayopelekewa mtu ili kumwomba ahudhurie katika sherehe, tafrija au hafla*, wakati tangazo ni *taarifa ya maandishi inayotolewa na mtu kupidia vyombo maalum ili kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi*.

Aidha, katika kipengele (b) waliweza kuandika tangazo linalohusu kumtafuta mtu aliyepotea kwa kuzingatia kichwa cha tangazo, jina la aliyepotea, wajihhi wake, maeneo anayopenda kutembelea, ahadi ya zawadi na mawasiliano kwa ajili ya kupokea taarifa ya anayetafutwa. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi kipengele (a) na (b) na kupata alama za juu.

	8. a) Barua yo mwaliko ni barua au maandichi yenye Tergo la kuumba ujio wa mtu fulani kwenye sherehe au chughuli yoyote maalumu takini tangazo ni maandichi yaliyoandikwa kwa madhumuni ya kutoa taarifa maalum kwa umma au walergwa mpango, nafaci za kazi, kupotea kwa mtu.
	<p style="text-align: center;"><u>KUPOTEA KWA MTOTO</u></p> <p>KIJANA WA KIUME AITWAYE MASANA      MADALE MWENYE UNINI WA MIKA 12      AMEPOTEA MAENEKO VA TENERU ARUSHA      SIKU YA TAREHE 12/12/2020 AKINA      AMEVAA CHATI YA BULUU NA CURUALI      NYEUCI KWA YEFOTE ATAKAYEMUONA      ATOE TAARIFA KWA KITUO CHA KARIBU      CHA POLICI AU APIGE NAMBA 0760626210      ZAWADI NONO ITATOLEWA KWA ATAKAYE-      FANI KICHA!</p>

Kielelezo Na. 8.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alieleza tofauti ya msingi kati ya barua ya mwaliko na tangazo kwa usahihi. Aidha, alimudu

kuandika tangazo la kupotea kwa *Masana Madale* kwa kuzingatia vigezo muhimu na kupata alama zote.

Hata hivyo, zaidi ya nusu ya watahiniwa (53.3%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyo jitoshleza katika kipengele (a) au (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kueleza tofauti ya msingi kati ya barua ya mwaliko na tangazo kwa kuandika *barua ya mwaliko huwa katika muundo wa barua* lakini *tangazo huwa katika muundo wa tangazo*; jibu ambalo si sahihi kulingana na tofauti bainifu inayoeleza kuwa; barua ya mwaliko ni *barua ambayo hupewa mtu au watu ili wahudhurie katika sherehe fulani* na tangazo ni *ujumbe unaotolewa kwa hadhira ili kutoa habari juu ya kitu fulani*. Aidha, mtahiniwa huyo katika kipengele (b) aliandika tangazo kwa usahihi japokuwa alibadilisha jina la aliyepotea kuwa *Masane Mandele* badala ya "Masana Madale", hivyo kupata alama za wastani.

Licha ya ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swalii hili, watahiniwa wachache sawa na asilimia 5.2 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kutoa majibu yasiyo sahihi katika kipengele (a) na (b). Watahiniwa hao, walishindwa kueleza kwa kifupi tofauti ya msingi kati ya barua ya mwaliko na tangazo katika kipengele (a) kutokana na kukosa maarifa stahiki. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; 'barua ya mwaliko' ni *barua ya kirafiki* na '*tangazo*' ni *barua ya kikazi*. Aidha, wengine walionesha kukosa uelewa kabisa wa dhana hizo, hivyo kutokuandika chochote kuhusiana na kipengele hicho kilichowataka kueleza tofauti ya msingi kuhusu dhana hizo kuwa, *barua ya mwaliko* ni barua ambayo hupewa mtu au watu ili wahudhurie katika sherehe fulani na *tangazo* ni *ujumbe unaotolewa kwa hadhira ili kutoa habari juu ya kitu fulani* kama vile kutangaza nafasi za kazi au vitu mbalimbali.

Vivyo hivyo, katika kipengele (b) walishindwa kuandika tangazo la kumtafuta ndugu *Masana Madale* aliyepotea ambapo baadhi yao waliandika *barua za kirafiki, kikazi na mialiko mbalimbali* na wengine walitoa taarifa zinazohusu wajihii wa aliyepotea bila kuonesha kuwa ni tangazo. Watahiniwa hao walitakiwa kuandika

tangazo linalozingatia kichwa cha tangazo, jina la aliyepeota, wajihii wake, maeneo anayopenda kutembelea, ahadi ya zawadi iwapo ipo na mawasiliano kwa ajili ya kupokea taarifa. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyokidhi matakwa ya swali.

<p>8. Barua ya mwaliko huwa na Anwani ya mwandishi hai na Anwani ya mwandishi lakini barua ya matang oza huwa na Anwani ya mwandishi.</p> <p><b>TANGAZO TANGAZO !!!!</b></p> <p style="text-align: right;">SHELUI SHULE YA SHELU SEKONDARI S.L.P 138; KIOMBOI - IRAMBA. 23 / 11 / 2020.</p> <p><i>Shule ya Shelui sekondari inowafungozi Kunzi Kijana Amepotea Katika hifiji cha shulek Kijana huyo anaishwe masana madale amepotea Eto ka wiki iliyapita asubuhili aliyoga anakwenda Shamboni hiyo hakurudi: tenzo nyim baati hadi sassi anaumii wa miaka kumi na tano, mfupi ni wa maji yo kunde ngozi yake amevaa tisheti ya bluu na sultuoii ya damu ya mzee na vratu vifunayo mala pa makundu hiyo baati atakoe bahati kwa kumwona atae tarifa kufuu cha polisi Vilichope kai bu nce au apige simu namba 0727121320 au 0612274761</i></p> <p style="text-align: right;"><i>SHELU SEKONDARI</i></p>
---

Kielelezo Na 8.2: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alieleza tofauti kati ya barua ya mwaliko na tangazo kuwa zote huwa na *anwani ya mwandishi* na katika kipengele (b) aliandika barua ya kirafiki ambayo ilikuwa na anuani ya mwandishi pamoja na kuweka saini mwishoni mwa barua hiyo kinyume cha matakwa ya swali.

## 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu C ilikuwa na maswali manne ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 45.

### 2.3.1 Swali la 9: Ukuaji na Ueneaji wa Kiswahili Baada ya Uhuru

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, mada ndogo ya *Ukuaji na Ueneaji wa Kiswahili Baada ya Uhuru* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutathmini mchango wa vyombo vya habari katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia vyombo vinne vya habari vilivyopo nchini hivi sasa kuonesha mchango wa kila kimoja katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 216,283 sawa na asilimia 49.4 ya watahiniwa wote walifanya mtihani. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 152,024 sawa na asilimia 70.3 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

#### Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya Wanafunzi
0.0 - 4.0	64,259	29.7
4.5 - 9.5	79,479	36.7
10.0 - 15.0	72,545	33.6

Katika Jedwali Na. 3, watahiniwa 64,259 (29.7%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4, watahiniwa 79,479 (36.7%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 72,545 (33.6%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15.

Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 36.7 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walifauli kwa kiwango cha wastani kutokana na kutumia baadhi ya vyombo vyahabari vilivyopo nchini hivi sasa na kueleza mchango wa kila kimoja katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Baadhi yao, walimudu kuelezea vyombo vyahabari viwili hadi vitatu kati ya vinne viliviyotakiwa kama vile; *magazeti, majarida, redio, runinga na mitandao ya kijamii*. Pia, watahiniwa wengine hawakuzingatia vipengele muhimu katika uandishi wa insha kama vile utangulizi na hitimisho hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa waliojibu swalii hili vizuri ambao ni sawa na asilimia 33.6 walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mchango wa vyombo vyahabari vilivyomo nchini hivi sasa katika kukuza na kueneza Kiswahili. Watahiniwa hao, waliweza kutumia vyombo vinne vyahabari vilivyopo nchini hivi sasa kuonesha mchango wa kila kimoja katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Vyombo hivyo ni kama vile; (i) Magazeti: mfano Mwananchi, Tanzania Daima (ii) Majarida: mfano Femina, Hakielimu, (iii) Redio: mfano, TBC Taifa, Redio Free Africa, (iv) Runinga: mfano, TV Tumaini, ITV, TBC1 na (v) Mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter na nyinginezo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kulijibu swalii hili, katika utangulizi alieleza maana ya kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili, katika kiini alieleza namna vyombo vyahabari vinavyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili na kutoa hitimisho linaloelezea mchango wa vyombo vyahabari katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya mipaka ya Tanzania. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa huyo.

9. Kukua kwa kiswahili ni kitendo cha kuongezeka kwa miscamiati ya lugha ya kiswahili. Kuenea kwa kiswahili ni tendo la kuongezeka kimathumizi kijigagacia nthini. Vyombo mabali mbalimbali uya habari vimecadilia na kuchangica kukua kwa kiswahili na kuenea nthini. Kwa namna tafautitafauti vyombo hiyo ni karaa vile radio, magazeti, runinga na majarida. Kwa kuanza na magazeti, haya ni makarasi yaliyochapishwa habari mbalimbali za pje na relasi ya achi. Magazeti haya huchapishwa kwa lugha uya kiswahili. Hiyo watu hupata kuyasem kwa lugha uya kiswahili. Ili imesadilia kukua kwa kiswahili kwaani watu wanaposoma kiswahili wanendelea kukua matumizi yake kwa kujua na kuongeza miscamiati zaidi mpare Mwananchi. Pia runinga, hizi kutumikwa kupitisha habari kwa giza ya picha na sauti habari hizi hutolewa kwa giza ya kiswahili ambayo atatu wanaposikia wanrapata kuendelea kujifunza kiswahili zaidi mpare katika TBC, ITV na STARTV ni mifano ya channeli zinazotumika kutolea habari kwa lugha uya kiswahili. Radio, hivi ni vyombo uya habari ambayo hutolea habari kwa sauti tu ambayo mtu hukua na kusikiliza kinachoeanglewa. radio zimecadilia kukua na kuenea. Kwa kiswahili kwaani habari hutolewa kwa lugha uya kiswahili hiyo mtu anaposikiliza arawaa kujifunza miscamiati mipyga ya lugha. Radio hutolea taarifa kupitia channeli mbalimbali. Kama SUA F.m., Radio Imani, Claude F.m.

Mwiche, kwa kutumia majarida mbalimbali yanayoundikwa kwa lugha uya kiswahili. Kama vile "fema" ambayo hutolea habari kuhusu taarifa tafautitafauti kama vile gonywa la ukirinwi. Kwa hiyo haya huseinlia kukua na kuenea. Kwa kiswahili pale mtu anapnyasoma na kule kusoma kuta mpa mtu hiyo uwesa wa kuelewa na kusoma vizuri zaidi na hiyo lugha hutolea na kuenea zaidi.

Kwa kuhitimisha vyombo hivi uya habari vimeonyesta mchango mku bwa zana kwani habari harsikili swi nthini Tanzania tu bali hata nthi nyungine za pje kwa hiyo kiswahili harsikika hata kwa mataifa menginie na wao hupata kujifunza kidogo kidogo hadi matikuu nao huanza kutumia na hiyo kuperua matumizi.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swalii la 9.

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutumia vyombo vinne vya habari vilivyomo hapa nchini hivi sasa kama vile; *magazeti: runinga, redio na majorida* na kuonesha mchango wa kila kimoja katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Aidha, katika maelezo yake alitoa mifano ya mashirika ya utangazaji wa habari yaliyopo hapa nchini.

Hata hivyo, watahiniwa wengine (29.7%) waliojibu swalii hili walifaulu kwa kiwango hafifu kutokana na kukosa uelewa wa kutosha kuhusu mchango wa vyombo vya habari vilivyopo nchini hivi sasa katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Baadhi yao, walitoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swalii. Kwa mfano, waliorodhesha vipindi vinavyorushwa na vyombo mbalimbali vya habari na wengine waliandika mambo yanayosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili kama vile; *kampeni za kisiasa, kuteuliwa kwa lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa, kutumiwa kufundishia na biashara*. Watahiniwa hao, walitakiwa kutumia vyombo vinne vya habari vilivyopo hapa nchini kwa sasa kama vile; *magazeti, runinga, redio, majorida na mitandao ya kijamii kisha kuonesha mchango wa kila kimoja katika kukuza na kueneza Kiswahili*. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swalii hili na kupata alama hafifu.

9 Kwa Kitumia aina nne za vyombo vy  
habari vilivyo po ndini hivi sasa na kuo  
resha mchango wa kila Kimya. Katika  
Kukurza na Kueneza Lugha ya Kiswahili  
Kiswahili Kilieesa na Kukurza ndini kua  
Kupitia vyombo mbali mbali. Kama vile  
Baraza la Mitihani la Taifa; baraza  
ili ilisaidia Kueneza na Kukurza lugha ya  
Kiswahili kua kuchapisha mitihani ya  
Vijouoni na Mashule ya Msingi na Shule  
za sekondari hiyo basi baraza la Mitihani  
ya Taifa ndiyo ilisaidia Kukurza na  
Kueneza Lugha ya Kiswahili.  
Taasisi ya Elimu ya watu wazima;  
nayo ilisaidia Kueneza na Kukurza kiswahili  
kua Kupitia Masono ya jioni ambayo  
faliyokuna yanatolewa kiba watu ambazo  
unlikuwa awajapata elimu hiyo basi ya  
elimu ya watu wazima ilisaidia Kukurza  
Lugha ya Kiswahili.  
Dini; dini nayo ilisaidia Kukurza na  
Kueneza kua Kiswahili kua kitumia una  
rabi waliansisha lugha yao ya Kiarabu  
na waingereza waliansisha lugha ya  
kikiristi hiyo dini nayo ilisaidia kueneza  
a kua Kiswahili.  
Elimu; Pia elimu ilisaidia Kueneza  
na Kukurza Lugha ya Kiswahili kua kutoa  
elimu ndani na pje ya ndi.  
Hiyo Kiswahili kitikuwa na kueneza lugha  
ya Kiswahili kupitia vyombo mbalimba  
li Dini, Biashara, Elimu, Baraza la mitihani  
la Taifa ndiyo ilisaidia Kiswahili kikue  
na Kueneza.


Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu bayo la mtahiniwa katika swali  
la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alitumia asasi zilizochangia  
kukua na kueneza kwa lugha ya Kiswahili kama vile; *Dini na Elimu*  
kinyume na matakwa ya swali. Aidha, alielezea taasisi za *Baraza*  
*la Mitihani la Taifa na Taasisi ya Elimu ya watu wazima* ambazo  
majukumu yake ni tofauti na vyombo vy ya habari viliviyotakiwa.

### 2.3.2 Swalii la 10: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi* na lililenga kupima Tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha usemi usemao, “Kauli za washairi ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii bora” kwa kutumia hoja tatu kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili alizosoma, na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa la kuchagua ambapo watahiniwa 252,110 sawa na asilimia 57.6 walichagua kulijibu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo watahiniwa 233,948 sawa na asilimia 92.8 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 8:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swalii la 10

Katika Chati Na. 8, watahiniwa 18,162 (7.2%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4, watahiniwa 58,203 (23.1%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 175,745 (69.7%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15.

Asilimia 69.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwani walionesha uelewa wa kutosha juu ya

uhakiki wa ushairi. Watahiniwa hao, waliweza kuthibitisha kuwa, "Kauli za washairi ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii bora" kwa kutoa hoja tatu kutoka katika diwani mbili walizosoma zikihusisha "Wasakatonge", "Malenga Wapya" na "Mashairi ya Chekacheka."

Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na watahiniwa hao katika diwani ya "Wasakatonge" ni pamoja na kupiga vita *uongozi mbaya, kuwa na demokrasia ya kweli, kupiga vita ukoloni mamboleo, kupinga matabaka na kufanya kazi kwa bidii*. Aidha, katika diwani ya "Malenga Wapya" walithibitisha usemi kwa kutoa hoja zinazoonesha umuhimu wa *kutatua matatizo katika jamii, kukuza uchumi, ukombozi wa kifikra na kuimarisha mapenzi na ndoa*. Vivyo hivyo, katika diwani ya "Mashairi ya Chekacheka" waliweza kutoa hoja kama; *kuhamasisha ukweli, kupinga unyonyaji, kutetea haki ya kila raia na kuhimiza maadili mema*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kuthibitisha namna kauli za washairi zilivyo nyenzo katika ujenzi wa jamii bora alitoa hoja zilizojitosheleza na kutumia mifano sahihi ya mashairi kutoka katika diwani hizo. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kutoa hoja zilizokidhi matakwa ya swali.

10. Nyenzo muhimu ni vitu muhimu am bawyo vinafya kupratwa ili kuwaza kuyenga kitu bora. Washairi ni nyenzo muhimu katika ujerzi wa jamii bora kwa kutumia diniwani mbi: "Malenga Wapya" iliyounditwa na TAKILUKI na "Wasakatonge" iliyoundit na na M.S.Khatibu. Iputayo ni jinsi wa shairi walivyo nyenzo muhimu katika ujerzi wa jamii bora.

Kwa kutumia dewani ya "Malenga Wapya" iputayo ni jinsi washairi walivyo nyenzo muhimu katika ujerzi wa jamii bora.

Kukemea vongozi mbaya, mshairi amekemea vongozi mbaya kwani unau disha maendeleo ya jamii nyuma. Hii imeneeshwa kwenvye shairi la "Puuzo"

"Unapokuwa na shida wao warakupuza,  
Wanajita kidadu kuitanya aji za,  
Wanajitanya hawayal:

Hii imeneeshwa kuwa vongozi hawasitiili za rhida za wananchi yaani wanazipuza kama vile hazina umuhimu. Hii sifa hadi katika jamii zetu kwani vongozi hawasitiili za mahitaji ya wananchi. Hii yeye mshairi arakomea jambo hili.

Kupinga matabaka, mshairi anapina ngaa matabaka yaliyopo tati ya watu matajiri na watu maskini. Hii imeneeshwa kwenvye shairi la "Punda"

"Toka ulipozaliwa, maishayo ni kizogo,  
...Hakika ulionewa, hubustahili kipigo.

10 Hi cnaonesha kuwa wati maskini hawat hamini-wi na wati matajiri. Hadi kwenye jamii zetu mara nyingo wati wa tabaka la chini huwa hawathamini-wi. Hivyo mshairi anapingia jambu hilo.

Kukemea mshairi amekeme a suala la rushwa kuani lcnarudisha maendeleo ya jamii nyuma. Ici cmeone shwa kwenye shairi la "Sukari"

"Wengi wamefedhehoka, sukari wanaopapa, ...Kama hujitambua, ni chungu ndugu sukari. Hi cnaonesha kuwa mshairi ni kitu am bacho kinawauumiza wati wengi sana na pia kina madhara mengi sana. Hadi kwa nge jamii zetu mshairi ipo na cnaafanya a na wati wengi sana ikiwemo viangozi na wananchi wa kawaida. Hivyo mshairi anabemea suala la mshairi ili kuuweza ku leta maendeleo katika jamii

Kwa kutumia diwani ya "Wasakat enge" ifuatayo ni jinsi washairi walayo nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii bora.

Kupinga mila pototi ya utekefaji wa usanawake. Mshairi anapingang na suala la uteketaji kwa usanawake kuani lina madhara mengi sana. Hi cmeone mshairi kwenye shairi la "Tohara"

Tohara, kua usanawambe, ni hatari,  
Madhara, kua wake ute, hushamiri,  
Hasara, ya peke yate, hudihiiri,  
Zinduka.

10. Hii cnaonesha kuwa uketetaji wa wanawake una madhara mengi sana uketetaji wa wan awake upo hadi katika jamii zetu na zinata madhara mengi sana kwa mwanamke. Hii yeye mshairi arapingana na jambo hili

Kukemea ukosepu wa uadilifu, mshairi anakemea suala la ukosepu wa uadilifu kwa viangozi wa dini. Hii cnaoneshwa kwenye shairi la "Wasodhambi"

"Wardari,

Misalabi na mayuka, na hohiba,

-- Mambu yao,

Unafiki -

Hii cnaoneshwa kuwa viangozi wa dini sia waadilifu kwanza wanassema mambu am bayo hafa waao hawayafanyi. Hii ipo hidi katika jamii yetu ya sasa. Hii yeye msa nis anakemea suala hili la ukosepu wa uadilifu.

Kupinga suala la uchu wa madaraka, mshairi anapinda suala la uchu wa madaraka baina ya viangozi. Hii cnaoneshwa kwenye shairi la "Tonge la Ugali"

"Wacapigena,

Warauumizana,

Warauwana,

Kua tonge la ugali.

Hii cnaonesha kuwa viangozi wa uchi wana uchu wa madaraka na mabotayari kufanya lolote ilie ili wawezo kupata

madaraka ya uchi. Hii yeye mshairi anapinda suala hili la uchu wa madaraka.

Kua ujumla mshairi husaidi sana katika ujenzi bora wa jamii. Hii yeye wanayamii wanapaswe kusoma kazi hizi za tariki ili kuweza kuelcmika.

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.1 mtahiniwa alijibu vizuri swali hili kwani alitoa hoja kama vile; *Kukemea uongozi mbaya, kupinga matabaka na kukemea rushwa* kwa kutumia diwani ya "Malenga Wapya". Aidha, katika diwani ya "Wasakatonge" alitoa hoja kama vile; *Kupinga mila potofu ya ukeketaji, Kukemea ukosefu wa uadilifu na Kupinga suala la uchu wa madaraka*. Pia, katika hitimisho lake alitoa wito kwa jamii kusoma kazi za wanafasihi ili kupata elimu itakayowasaidia katika ujenzi wa jamii bora.

Hata hivyo, watahiniwa wengine (23.1%) waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja pungufu au zisizojitosheleza kutoka katika diwani husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa hoja halisi kutoka katika diwani ya "Wasakatonge" kama vile; *uongozi mbaya, demokrasia ya kweli na kupinga matabaka* lakini baadhi ya mifano ya mashairi aliyotoa hayakuwa halisi hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (7.2%) waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwani walionesha kuwa na uelewa mdogo juu ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi hasa katika kipengele cha Ushairi. Watahiniwa hao, walishindwa kuthibitisha usemi usemao, "*Kauli za washairi ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii bora*" kwa kutumia hoja tatu kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili walizosoma. Baadhi yao, walishindwa kuthibitisha usemi huo kwa kutoa hoja zilizohusu; *matumizi ya taswira, matumizi ya misemo, matumizi ya tamathali za semi* na wengine walieleza kinadharia maana na matumizi ya vipengele vya muundo/mtindo vinavyotumika katika ushairi kama vile *vina, mizani, utoshelevu na ridhimu* hivyo kupata alama hafifu. Watahiniwa hao walitakiwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili walizosoma kati ya "Wasakatonge", "Malenga Wapya" na "Mashairi ya Chekacheka." Kielelezo Na.10.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata 0.

10.1 Kwa Kumaluzi diwani ya WASAKATONGE  
 mwandishi ameonyesha kauli mbalimbali.  
 Tawiria ni picha anayaminyes ha mbunzi  
 na kazi la sahihi kwa tingo la kufikirisha  
 ujumbe kabdiwani mwandishi ameonyesha tar  
 jikatika shairi la MAHABA pale anaparema,  
 Nahodha  
 Wang'angani sukani,  
 Abiniya ujala bwabajeeka,  
 Psetka kulewa na kusapika,  
 kuapika, Nangoma zahata ka.  
 Mwandishi anadhitisha wa viangozi wan  
 avyo ng'ang'ania madaraka na rai kubareka.  
 Tashihisi, ni tamathali ya remi ambayo  
 hukypa kuu upendo ungofanya na binadamu.  
 Tashihisi diwani mwandishi ameonyesha tashihisi  
 si kabka shairi la MAHABA pale anaparema  
 kama mahaba waqimu, Nahiyari niazomene  
 Mwandishi amefananiha mahaba ni waqimu  
 na nikibu kisicho wezekana na pia angurisi  
 biza umuhimu wa mapenzi ya kweli.  
 Kejeli, ni ma meno ambayo  
 xanankashifu mby. kabka shairi mwandishi  
 ameonyesha kejeli kupihia shairi la kosa  
 pale anaparema  
 kera leby kubwa  
 kudai hakii?  
 Yehu mili ki.  
 Muna hamaki  
 Nahukumunabukashifu  
 Mwandishi ameonyesha jinsi viangozi wanau  
 vo wakashiru rai waao.


Kielelezo Na.10.2: Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swalii la 10.

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi ambapo katika diwani ya "Wasakatonge" alitoa hoja kama vile; *tawiria, tashihisi* na *kejeli*; hoja zinazohusu vipengele vya matumizi ya lugha kwenye kazi za kifasihi badala ya kuonesha jinsi ambavyo kauli za washairi ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii bora.

### 2.3.3 Swali la 11: Uhakiki wa Riwaya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua na kutathmini maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli kuwa, "Jamii ya Kitanzania inakabiliwa na matatizo mbalimbali ya kijamii yanayokwamisha maendeleo" kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya katika ya riwaya mbili alizosoma. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa la kuchagua ambapo watahiniwa 413,727 sawa na asilimia 94.5 ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua kulijibu. Hili ni swali lililojibiwa vizuri zaidi ambapo watahiniwa 393,083 sawa na asilimia 95.0 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



Chati Na. 9: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11

Katika Chati Na. 9, watahiniwa 20,644 (5.0%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4, watahiniwa 74,265 (18%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 318,818 (77.0%)

walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15.

Asilimia 77.0 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walifanya vizuri kutohana na uelewa wa riwaya teule waliokuwa nao na maarifa toshelevu kuhusu uhakiki wa maudhui katika riwaya hizo. Watahiniwa hao, waliweza kuthibitisha kauli kuwa, “Jamii ya Kitanzania inakabiliwa na matatizo mbalimbali ya kijamii yanayokwamisha maendeleo kwa kubainisha matatizo sahihi yanayopatikana katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" kwa kutoa hoja kama vile; *wanaume kutokuwajibika katika malezi ya familia, madawa ya kulevyaa, umaskini na ulevi uliokithiri*. Katika riwaya ya "Takadini", walibainisha matatizo kama vile; *kunyanyapaa ugumba na utasa, walemavu wa ngozi, kuchagulia watoto wachumba na ndoa za mitala*. Pia, katika riwaya ya "Joka la Mdimu" walibaini matatizo kama vile; *uhujumu uchumi, hali ngumu ya maisha, rushwa na uzembe kazini*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alithibitisha kauli hiyo kwa kutumia riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" na kutoa hoja kama vile; *tatizo la umaskini, ulevi, madawa ya kulevyaa* na katika riwaya ya "Takadini" alieleza kuhusu *mila potofu, tatizo la ndoa za mitala* na *wivu*. Kielelezo Na.11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swalii hili na kupata alama za juu.

11. kwa telanzia na riwaya ya "Watoto uva Mama N'tilie" nsiyandibea na Emmanuel Mbogo yaphakayo ni malitizo valiyojitobeza kuonye riwaya hiyo.

Wizi na Ujambazi: Wizi na ujambazi ni hali au namna ya kupora na kuchukua mitu wya mmilika pagipo na ridaa ya mmilika. Wizi na Ujambazi unaoyeshua na kuluu, Doto na Dan walipacawaa kuiba kuonye aluba ja muhindi na kuchia kopo nti pindi walipopiguo bactola na mlizi uva lindo hiyo. Tat thili ni tatizo linatalukamicha maendeleo kwenye kipanga mmilika kipotora mali zake kipolekeba umarikini na pindi wezi au majambo yaao wanaposiwa na nchi kipotora ngumu lazi na tifyo kubiamicha masteleo.

Utarri: Utari iraonyeshua kazi na mzee Tomotero babu uva Peter and Rita. Mzee Tomotero alikuwa hachangii kitu chochote buonye familiya na jani yake kazi yake kumyua pombe na chang'aa na tifyo kipanga watoto waachindwe kuenda shule bucini wadi. Kuwa walimtagomea mama yao pekee atibae bijato shahabu habikua aki kitukuu pia tifyo kuhua micha maendeleo. Wanajamii hewi wengi hua watovi hadala ya kuchangia batiba kufunga taifa lao kua kipanga lazi na tifyo kipolekeji kuhawamicha maendeleo.

Utospu wa elimu, ni hali ya kuhapata elimu. Hili tathilo ni janiga kubwa sana bucini mitu akisepo elimu arakwaa hana uweso uva keter kujikombaa kichumi 3iraonyeshua hili na anti E. mbogo kua kuhuni

11. Musa, kijana aliyotosa elimu na baadaye kujihus  
isha na madawa ya kulonya na kuichia mitoni  
ni mua akteria - hivyo kuboamicha maendeleo  
ya jamii.

"kutumia nivaya ya "Joka la Mdimu" napustay  
ni matatizo yanayobuoamicha maendeleo.

Rushwa, ni hola au biamu ya kitu chechote  
kutakwachio ili kupata tukuma ya haraka ambayo  
hawatuhiki, au bukuope tuhuma na machakila.  
muaridishi anaompeha tafizo hili dhahiri kwa  
kumtumia Tino na daktari • Tino ilibidi atoo rushwa  
a kua daktari ikitumwezasha mtoto uake atibewe  
nje ya rohi. Rushwa inabuoamicha maendeleo buani  
kifaa mtu orapohitaji kitu hata kama ni kati yabo  
lazima atoo kiti ili kumupashia mtu mwengine na  
kumuumiza mtu mwengine na hili huleta au na huba  
micha maendeleo ya jani

Utesafu wa uadilifu wa viongozi. Viongozi wa  
famii kubwa uadilifu na kufanya taizi zito vile  
icihyotabuwa na hili kuleta ukosefu wa maendeleo  
ya jamii mpano ilibuuwa ni taizi ya daktari kum  
vandiliza mtoto wa Tino aende hajipatalini labini  
habuandika hilo mpaka aliyopata kitu kinachem  
hupashia moye hivyo wao ambaa hadana uwazo  
wa kutoa kifo aei anaohobatibia kiongozi huchindua  
kupata kati 200 • ni pia viongozi ualivopewa madaa  
ka bedala ya kuleta maendeleo buenyi jamii hiyo  
nya maisha yauye magumu.

Biasara haramu na uendaji haramu. Uendaji haramu  
mu ni kuiwinda ne wainmama peri na kuchukua napzi  
na pembe zao. pasipo na bibali kustoka serébalini  
na basdae kuziwa.

Kielelezo Na.11.1: Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali  
la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.1, mtahiniwa alitoa hoja tatu kila  
riwaya. Katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tiliye" alibaini kwa  
usahihi matatizo kama vile; *wizi na ujambazi, ulevi na ukosefu wa  
elimu*; na katika riwaya ya "Joka la Mdimu" alitoa hoja kama vile;  
*rushwa, ukosefu wa uadilifu wa viongozi, biasara haramu na*

*uwindaji haramu* ili kuthibitisha kauli isemayo, "Jamii ya kitanzania inakabiliwa na matatizo mbalimbali ya kijamii yanayokwamisha maendeleo."

Aidha, asilimia 18 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa waliweza kubaini baadhi tu ya changamoto zilizoko katika riwaya teule na nyingine zikiachwa. Hivyo, majibu yao yalikuwa hayajitoshelezi kwa hoja na mifano katika riwaya teule na kusababisha kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua matatizo sahihi katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" lakini alishindwa kubaini baadhi ya matatizo katika riwaya ya "Takadini" kwa kuandika suala la *wizi* na *ujangili* tatizo ambalo halikuzungumziwa katika riwaya hiyo bali hupatikana katika riwaya ya "Joka la Mdimu."

Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 5.0 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Ufaulu huo ultokana na kukosa maarifa ya kuchambua maudhui katika riwaya teule ili kuthibitisha kauli isemayo, "Jamii ya Kitanzania inakabiliwa na matatizo mbalimbali ya kijamii yanayokwamisha maendeleo". Baadhi yao, walichambua vipengele vya fani kwa kueleza *migogoro* na *wasifu* na *wahusika mbalimbali* kutoka katika riwaya teule bila kuhusisha na changamoto ambazo ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii kwa jumla. Mfano, mtahiniwa mmoja alimwelezea mhusika *Mama N'tilie* kutoka katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" kuwa ni *mwema na mlezi bora* lakini alishindwa kuonesha ni namna gani ameshindwa kutekeleza majukumu ya malezi ya watoto wake kutokana na kukosa ushirikiano kutoka kwa mumewe Lomolomo, hivyo kupata alama hafifu.

Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja zisizokidhi matakwa ya swalii kwa kuandika maswala yanayohusiana na mada za *Sarufi* na *Matumizi ya Lughu*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuhusu *umuhimu wa misimu katika lugha* kama vile; *kuongeza msamiati na kupamba lugha* badala ya kubainisha matatizo mbalimbali ya kijamii yanayokwamisha maendeleo kama yalivyoibuliwa na waandishi kutoka katika riwaya teule kama vile;

wanaume kutokujibika katika malezi ya familia, madawa ya kulevyo, umaskini na ulevi uliokithiri kutoka katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie"; unyanyapaa wa ugumba na utasa, unyanyapaa wa walemvu wa ngozi, kuchagulia watoto wachumba na ndoa za mitala kutoka katika riwaya ya "Takadini" na uhujumu uchumi, hali ngumu ya maisha, rushwa na uzembe kazini kutoka katika riwaya ya "Joka la Mdimu." Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibinisa migogoro kutoka katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" kinyume cha matakwa ya swali na kupata alama hafifu.

11	<p>Jamii ya vifundani mhabitiwa na matatizo mbili: mbali ya kijamii yanayop kumemeza matendeleo. "Thiki husha kauli hii kwa kutea hejo kwa kila msingi kati ya riwaya mbili ulizosoma.</p> <p>Nikianza na msingi ya mama n'tilie kicheo ndelewa na E. mbege (H-r-P) ziquatalo ni hujaa riwaye ya mama n'tilie.</p> <p>Migogoro kati ya Dotc na jeteri, mgogoro huu ulisababishwa ba'palo dotc alipokuwa anataku kula atupeka aqai jeteri haku fuchishwa na kilekilendwa chake kura kumepi na mgogoro huu ni; kauli ya kwa na msho usye na msingi kati kuu hadhi fulan fuluhisho hili linapoleko palo Dotc na jeteri walipu kuna, uia na fe rawa elimu na mama n'tilie.</p> <p>Mgogoro kati ya zita na kura, mgogoro huu uli sababishwa pala kuewa alipu ilimwa na kipalo kura hasp tali na shingai alipu mtaridha kura alipewmwa na ilengenjwa use jukisang baada ga siku ziquatalo mama yao alipeweli hako saremi wali muhaditha ku husu mtaa masha yao na shingai.</p> <p>Mgogoro wa kinafsi, mgogoro huu ulisababishwa ba'palo tendi alikuwa na kinafsi alipetuwa na watoto wa mama n'tilie mbilyo ya kuna sareki.</p>
----	---


Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa alibainisha migogoro mbalimbali iliyojitokeza katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" kama vile; *mgogoro kati ya Peter na Doto, mgogoro kati ya Zita na Kurwa na mgogoro wa kinafisia* badala ya kubainisha matatizo mbalimbali ya kijamii yanayokwamisha maendeleo yaliyoibuliwa na watanzi wa riwaya teule. Hata hivyo, mtahiniwa huyo hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu riwaya hiyo kwani alichanganya majina ya wahusika kwa kuwatumia *Shingai* na *Tendai* ambaao ni wahusika wanaopatikana katika riwaya ya "Takadini"

#### **2.3.4 Swali la 12: Uhakiki wa Tamthiliya**

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini maandishi ya kifasihi hususan tamthiliya teule. Swali lilimtaka mtahiniwa kutetea kauli kuwa, "waandishi wa kazi za fasihi hulenga kuleta mabadiliko katika yale wanayoyaandika" kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili walizosoma. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa la kuchagua ambapo watahiniwa 365,940 sawa na asilimia 83.6 walilijibu. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri ambapo, watahiniwa 340,478 (93.0%) walifaalu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.



**Chati Na. 10:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12

Katika Chati Na. 10, watahiniwa 25,462 (7.0%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4, watahiniwa 86,442 (23.6%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 254,036 (69.4%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, watahiniwa wengi sawa na asilimia 69.4 walijibu vizuri kwani walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uhakiki wa tamthiliya teule. Hivyo, waliweza kutoa hoja sahihi zenyе kutetea kauli kuwa "waandishi wa kazi za fasihi hulenga kuleta mabadiliko katika yale wanayoyaandika" kwa kutumia tamthilia teule "Kilio Chetu, Orodha na Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe". Mabadiliko yaliyolengwa na waandishi na kuelezw na watahiniwa hao ni pamoja na *wazazi kuwapa watoto wao elimu ya jinsia, vijana kutojihusisha na mapenzi katika umri mdogo, wanandoa kuacha tabia ya kusaliti ndoa zao na watoto kuacha tabia ya kuangalia picha za X (ngono)* kutoka katika tamthiliya ya "Kilio Chetu". Aidha, katika tamthiliya ya "Orodha" waliweza kuonesha mabadiliko ya jamii yanayolenga kuondokana na *ulevi, umaskini, kujinusuru na janga la UKIMWI, usaliti katika ndoa na mwenendo usiofaa wa viongozi wa dini*. Pia, katika "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" walionesha mabadiliko yanayolenga kuondokana na

*kuchanganya mapenzi na kazi, ulevi na tabia ya kuamini imani za kishirikina.* Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri na kupata alama za juu.

Kua kuanza na tamthiliya ya "Kulio chetu" mwandishi ameweza kuthibishsha kauli hii kama ifuatavyo,

Elimu ya kijinsia yapaswa kutolewa kwa watoto, mwandishi anaonyesha kuwa jamii inabidi ibadilike kua kuanza kutoa elimu ya kijinsia kwa watoto. Mfano, Suci alijipigiza kahiko mapenzi katika umni mdogo hiyo kupata mrimba na kuwa kuwa alikosa elimu hiyo ya jinsia. Jamii yapaswa kufanya mabadiko kua kutoa elimu ya jinsia kua watoto.

Kuacha mila potofu, jamii yapaswa kuhadilika kua kuacha mila potofu ambazo bukwamisha maendeleo. Mfano Wasabi wa Johi waliamini kuwa Johi amchagua ndio maana anasumbulia na maradi. Mwandishi anataka jamii ibadilika ha io kua kuachana na mila hizi potofu.

Kuwa na msimamo, jamii yapaswa kuwa na msimamo katika jambo ili kuweza kufanikwa. Mfano, Ana alikuwa na msimamo wake ya kwamba hataki kuijhuisisha na mambo ya kumapensi kahika umni mdogo. Mwandishi anataka watu wawe na msimamo ili wawex kufanikiwa.

Vilevile kahika tamthiliya ya "Orodha" mwandishi ameweza kuthibishsha kauli hii kama ifuatavyo.

Kuachana na vitendo vya usherah, jamii yapaswa kutambua vitendo vya usherah

12. huwa na madhara makubwa. Mfano Furaha na Mary walijhusisha na vitendo vya uasherati na hiyo kuperelkeo Furaha kupata UKIMWI. Jamii yapaswa kujihadilisha na kuacha tabia hii mbaya.

Kuwa na maadili mazuri, jamii yapaswa kuwa kuwa maadili mazuri ni msingi wa maisha Mfano. Furaha alikuwa akitorokwa nyumbani usiku na kwenda baq na halimaye kupata UKIMWI. Mwandishi anataka mali wabadiiliko na iwe na maadili mazuri.

Kuwa muaminifu, jamii yapaswa kutambaa kuwa yaminifu ni taji lenye faida. Kubwa sana na hujulikao madhara mengi pindi ambapo wapi hawatofuata. Mfano, Padri James alimjonyo Furaha alale nne ikiwa ni njia ya kumtamani badala ya kumsaidia Furaha kuthibui madhambhi yako Jamii yepesi. Mwandishi anataka jamii ibadiiliko na iwe na yaminifu baddla ya kufanya hijana ili kupelekeo maendeleo.

Hivyo basi, waandishi yoa kazi za fasihi hulenga kuleta mabadiliko katika yale wanayoandikia. Hatuna pudi kukubali mabadiliko haya ili kuweza kuleta maendeleo katika jamii.

Kielelezo Na. 12.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swal la 12.*

Katika Kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa aliweza kutetea kauli kuwa waandishi wa kazi za fasihi hulenga kuleta mabadiliko katika yale wanayoyaandikia kwa kutoa hoja katika tamthiliya ya “Kilio chetu” kama vile; *umuhimu wa elimu ya jinsia, kuacha mila potofu na kuwa na msimamo*. Pia, katika tamthiliya ya “Orodha” alitetea kwa kutoa hoja kama; *kuachana na vitendo vya uasherati, kuwa na maadili mazuri na kuwa muaminifu katika jamii*. Aidha, katika kuhitimisha alisisitiza jamii kukubali mabadiliko yanayoandikwa na waandishi ili kuleta maendeleo katika jamii.

Vivyo hivyo, asilimia 23.6 ya watahiniwa waliojibu swalii hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kutetea kauli kuwa, "waandishi wa kazi za fasihi hulenga kuleta mabadiliko katika yale wanayoyaandika". Watahiniwa hao, walionesha uelewa sahihi wa matakwa ya swalii japokuwa baadhi yao walitoa hoja pungufu na wengine walishindwa kutumia mifano sahihi ya ushahidi kutoka katika tamthiliya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kuhusu *mabadiliko ya jamii dhidi ya mienendo isiyofaa ya viongozi wa dini* lakini alishindwa kuonesha mhusika wa jambo hilo ambaye ni *Padri James* kutoka katika tamthiliya ya "Orodha," hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (7.0%) pekee ndio walioshindwa kutetea kauli kuwa, waandishi wa kazi za fasihi hulenga kuleta mabadiliko katika yale wanayoyaandika kwa kuwa na uelewa mdogo kuhusu uhakiki wa tamthiliya teule. Baadhi yao, walitoa hoja zinazohusu fasihi kwa ujumla, hususan dhima za fasihi, tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi na fani na maudhui katika kazi za fasihi. Wengine walizungumzia tanzu na vipera vya fasihi simulizi badala ya kuonesha mabadiliko ya jamii kama yalivyoandikwa na waandishi kutoka katika tamthiliya teule. Mabadiliko hayo ni kama vile; *watoto kupata elimu ya jinsia, vijana kutofanya mapenzi katika umri mdogo, wanandoa kutosalitiana na watoto kutoangalia picha za ngono kutoka katika tamthiliya ya (Kilio Chetu), jamii kuondokana na ulevi, umaskini, kujinusuru na janga la UKIMWI, usaliti katika ndoa na mwenendo usiofaa wa viongozi wa dini* (Orodha) na kuondokana na *kuchanganya mapenzi na kazi, ulevi na tabia ya kuamini imani za kishirikina* (Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo na mashiko kwa kuandika *maana ya fasihi simulizi* kisha kutoa utangulizi wa kujibu swalii kwa kutumia tamthiliya ya "Kilio Chetu" na "Orodha" lakini akatoa hoja zisizohusiana na tamthiliya hizo kama Kielelezo Na. 12.2 kinavyodhihirisha sehemu ya majibu ya mtahiniwa huyo.

12. Tafiti Ni sana ambayo ihatumia lugha  
Makutu Mafuta Kipiptoo Ijumbe Una waadiliko  
au jamii pia. Kuhatumia tamthiliya  
mbili Ambaro ni "Orodha" Uyoandikuni na  
Steve Reynolds na "Kilio Chetu" Wilchoandikuni  
na Medikal Aid Foundation. Kuhatumia na  
tamthiliya ya "Orodha" muandishi Steve  
Reynolds yajifatako ni mabadiliko yanayoleta  
o na tamthiliya.

Muelimisho jamii. Kuhatumia tamthiliya  
ku muandishi Ametera mabadiliko ya  
Maya telo Unaoma. Tamthiliya Kuelimisho kienye  
pi Una waatirisha kutu Chetu tamthiliya  
waatirisha na baada ya kopo Una kienye kidogo  
wana chini kie Una kienye kilehuu.

Multsoa jamii. muandishi wa tamthili  
amezengumto Kuturu swali la Multsoa  
jamii Mafuta Junia la Mafuta jamii  
muandishi anauye Unaoma tamthiliya  
Una kienye aridhia na anauye kupo  
la Ijumbe tig Ilama Alifunua ana to  
biu mbaya Kuwalintepo tamthiliya ana  
anauye aktarimiki.

Maburudisha jamii. Muandishi wa tamthili  
hi hii anaburudisha Una Kipiptoo misangi  
yajifatako anaburudisha pale ambayo atakuna  
na Kipiptoo mabmo ambayo yanakeisho nli  
o atakunudika Kipiptoo aya na fofari.  
Nila Una Kipiptoo mambayo pale o  
mbayo atakuna na Unaoma habia yake  
liko kilehuu na tudio atakunuki ci  
Kipiptoo Mayayo

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya sehemu ya jibu baya la mtahiniwa  
katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.2, mtahiniwa alijibu kinyume na matakwa  
ya swali kwani alielezea dhima mbalimbali za fasihi kama vile;  
*kuelimisha jamii, kukosoa jamii na kuburudisha jamii* kwa kutumia  
tamthiliya ya "Kilio Chetu" na "Orodha" badala ya kuonesha  
mabadiliko yaliyolengwa na waandishi wa tamthilia hizo.

### **3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA**

Mtihani wa somo la Kiswahili ulihuisha maswali 12 yaliyotahiniwa katika mada ya *Ufahamu*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utumizi wa Lughu*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili na Fasihi*.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa, watahiniwa walifaalu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri katika mada zote zilizotahiniwa mwaka 2020. Kiwango hicho kiliongozwa na mada ya *Uandishi* (94.8%) iliyotahiniwa katika swali la 8. Mada hii ilifuatiwa na mada ya *Fasihi* (91.6%) iliyotahiniwa katika swali la 2, 6, 10, 11 na 12, *Utumizi wa Lughu* (90.2%) katika swali la 5, *Maendeleo ya Kiswahili* (70.3%) katika swali la 9 na mada mchanganyiko (72.9%) zilizotahiniwa katika swali la 1. Mada zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ni; *Ufahamu* (44.3%) iliyotahiniwa katika swali la 7 na *Matumizi ya Sarufi* (39.4%) iliyotahiniwa katika swali la 3 na 4.

Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, katika mtihani huu kulikuwa na mada ambazo kiwango cha ufaulu kiliongezeka na nyingine kushuka. Mada tatu zilizokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa mwaka 2020 zilionesha kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu ikilinganishwa na mwaka 2019. Mada hizo ni; *Uandishi* iliyokuwa na ongezeko la asilimia 21.6 kutoka (73.2%) hadi (94.8%), *Fasihi* kutoka (80.2%) hadi (91.6%) ikiwa ni ongezeko la (11.4%) na *Maendeleo ya Kiswahili* kutoka (56.6%) hadi (70.3%) sawa na ongezeko la asilimia 13.7. Uchambuzi huu unaonesha kuwa, kwa ujumla mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa jumla umeimarika zaidi.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, ufaulu wa mada tatu ulishuka ikilinganishwa na mwaka 2019. Mada hizo ni pamoja na *Mada Mchanganyiko* iliyopungua kwa asilimia 12.8 kutoka (85.7%) hadi (72.9%), *Ufahamu* kutoka (81.2%) hadi (44.3%) ikiwa na upungufu mkubwa wa asilimia 36.9 na *Sarufi* kutoka (51.8%) hadi (39.4%) ikiwa pia imepungua kwa asilimia 12.4.

Wastani wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada zote kwa mwaka 2020 ni asilimia 71.9, kiwango hiki ni cha juu kidogo kwa asilimia

0.4 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo wastani wa kiwango cha ufaulu kwa mada kilikuwa 71.5%. Hivyo, kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2020 kinaonesha kuwa, watahiniwa wengi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa.

Kwa jumla, mada zilizokuwa na kiwango cha chini cha ufaulu kwa mwaka 2020 ni mada ya *Sarufi* kutokana na watahiniwa wengi kukosa maarifa mahsusui kuhusu mada ndogo ya *Aina za Maneno*. Hivyo, kushindwa kupambanua mazingira ya vielezi katika lugha ya Kiswahili. Pia, watahiniwa walionesha kukosa umahiri wa kuelewa vifungu vya ufahamu vinavyotokana na ushairi, hivyo kushindwa kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho.

Hata hivyo, mada zilizokuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani (*Ufahamu na Sarufi*) zinatakiwa kutiliwa mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wake ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa maarifa na kuwafanya kuwa mahiri katika somo la Kiswahili. Ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2020 umeainishwa katika **Kiambatisho A**. Pia, ulinganifu wa viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika mada kwa mwaka 2019 na 2020 umeainishwa katika **Kiambatisho B**.

#### 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Mtihani wa Kidato cha Nne katika somo la Kiswahili mwaka 2020 ulizingatia Muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani *kukumbuka, kuelewa, kutumia, kuchambua, kutathmini na kuunda*. Kiwango cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa kizuri ambapo asilimia 94.83 ya watahiniwa walifaalu somo hili.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile; kutofuatwa kwa maelekezo ya swali na uelewa mdogo wa baadhi ya mada hususan mada ya *Sarufi* na *Ufahamu*. Hata hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa, zipo mada zinazohitaji jitihada za dhati katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii ni kwa sababu kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada ya *Sarufi* kimeendelea kushuka kwa miaka mitatu mfululizo ambapo mwaka 2018, kiwango cha ufaulu kilikuwa (64.1%), mwaka 2019 (51.8%) na mwaka 2020 (39.4%), kiwango ambacho ni cha

chini zaidi ikilinganishwa na miaka miwili iliyotangulia. Aidha, mada ya *Ufahamu* (43.3%) imekuwa na ufaulu wa chini kwa mwaka 2020 ikiwa na upungufu mkubwa wa asilimia 36.9 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Mwisho, taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Kiswahili na kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hali hii itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayosababisha ufaulu wa kiwango cha chini ili kuweza kufanya marekebisho kwa ajili ya kuinua kiwango cha kufaulu kwa kipindi kingine.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili hususan kwa mada ya *Sarufi* na *Ufahamu* zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu inashauriwa kuwa:

- (a) Ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya *Sarufi* uzingatie zaidi matumizi ya mbinu shirikishi na kutoa mazoezi ya kutosha kuhusu ufanuzi wa aina mbalimbali za maneno.
- (b) Walimu wawaongoze wanafunzi katika kusoma vifungu vya habari/mashairi na matini mbalimbali za lugha ya Kiswahili kwa ufhamu ili waweze kujibu kwa ufasaha maswali ya ufhamu yanayotokana na vifungu vya habari au ushairi.
- (c) Walimu watumie njia ya majadiliana na vielelezo vya kufundishia (zana za kufundishia) zinazopatikana katika mazingira halisi. Aidha, mada zote zifundishwe kwa vitendo ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi kwa kulinganisha anachofundishwa na uhalisia wake.
- (d) Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya kutosha wakati wa kujifunza na kuwapa mrejesho. Hii itasaidia kubaini na kuondoa udhaifu katika maeneo ambayo wanafunzi hawakuelewa vizuri mada husika.
- (e) Walimu wasisitize wanafunzi kusoma vitabu vya kiada, ziada na matini mbalimbali za kifasihi na zisizo za kifasihi ili kuwajengea umahiri katika kuelewa dhana mbalimbali za kisarufi na kifasihi.

## KIAMBATISHO A

### UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Na.	<i>Mada</i>	Ufaulu kwa kila Swalii		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni
		Na. ya Swalii	% ya Ufaulu (alama 30 <sup>+</sup> )		
1.	<i>Uandishi</i>	8	94.8	94.8	Vizuri
2.	<i>Fasihi</i>	2	92.8	91.6	Vizuri
		6	84.6		
		10	92.8		
		11	95		
		12	93		
3.	<i>Utumizi wa Lugha</i>	5	90.2	90.2	Vizuri
4.	<i>Sarufi, Utumizi wa Lugha na Fasihi kwa ujumla (Swali la Kuchagua)</i>	1	72.9	72.9	Vizuri
5.	<i>Maendeleo ya Kiswahili</i>	9	70.3	70.3	Vizuri
6.	<i>Ufahamu</i>	7	44.3	44.3	Wasta ni
7.	<i>Sarufi</i>	3	45.2	39.4	Wasta ni
		4	33.6		

## KIAMBATISHO B

### ULINGANIFU WA VIWANGO VYA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI KWA MWAKA 2019 & 2020

